# Nipashe

Jumatano Januari 13, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580459

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Sakata** la mwanafunzi kudaiwa kubakwa na mwalimu latua kwa DC

UKURASA 3



**Bei** ya samaki wa kukaangwa juu kisa mafuta

UKURASA 3




**Dybala kukosa mechi muhimu za Juventus**

UKURASA 20

# Shehena mafuta kula yatua kuokoa uhaba

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisalimiana na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, wakati wa sherehe za maadhimisho ya miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jana. Wengine ni mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi na Mama Fatma Karume, mjane wa Hayati Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa SMZ. **Picha zaidi uk. 7. PICHA: IKULU ZANZIBAR**

## Lukuvi apiga 'stop' viongozi kuuza ardhi

UKURASA 2

## Dk. Mwinyi aagiza fedha za Mapinduzi zipelekwe elimu

UKURASA 17

**MICHEZO** **MIRAJI ANUKIA KIATU MAPINDUZI CUP** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Shehena mafuta ya kula yatua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, amesema hali ya upatikanaji wa mafuta ya kula inatarajiwa kutengemaa hivi karibuni baada ya meli ya pili iliyobeba shehena ya tani 26,450 kutua katika Bandari ya Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Waziri Mwambe, meli hiyo ilitia nanga Januari 5, mwaka huu na ratiba ya ushushaji wa shehena inaonyesha Januari 19 hadi 22 mwaka huu, Mwambe akiahidi kuwasiliana na Waziri wa Uchukuzi ili shehena hiyo ipakuliwe haraka.

Aliwahakikishia Watanzania kuwa serikali itaendelea kuhakikisha mafuta yanapatikana kama ambavyo imepangwa.

"Hii meli ya pili inayoshusha mafuta hivi karibuni nimeshawasiliana na waagizaji wake, meli zingine zitakuja siku 45 zijazo.

"Kwa mwezi, tunatumia Metric Tonne 30,000 kama nchi tunayoagiza kutoka nje, acha tunayozalisha huku ya alizeti, karanga na nazi, tutahakikisha mafuta yanakuja, hatukwami," alisema.

Alisema suala lingine ni kutoa upendeleo kwa meli zinazokuja za mafuta ili yasiadimike kwa sababu ya kuchelewa kutia nanga.

"Tutatengeneza ratiba ya kuwezesha kushushwa mafuta ya kula mapema maana gati linalotumika kushusha ndilo linalotumiwa kushusha petroli, dizeli," alisema.

Waziri huyo alisema tayari amezungumza na waagizaji wa mafuta kuhusu uwezo wa kuzalisha mafuta nchini na wamekubali kuandika barua ya kupatiwa mashamba makubwa ya kulima michikichi, kununua karanga na nazi, ili kuzalisha mafuta ya kutosha ndani ya nchi na kuondokana na uagizaji wa mafuta nje ya nchi.

"Kuna tofauti kati ya uhaba wa mafuta na kupanda kwa bei, mafuta yapo isipokuwa bei zimeongezeka kidogo, imetokana na hali halisi ya uzalishaji na usambazaji wa mafuta duniani, tumeona tangu Julai 2020, bei zimekuwa zikipanda katika soko la dunia.

"Oktoba bei ya mafuta ilifikia Dola za Marekani 786 kwa tani moja hadi inafika nchini. Kwa mwezi huu Januari, imefika Dola za Marekani 1,075 kwa tani moja na imetokana na sababu nyingi, kubwa ni ugonjwa wa corona licha ya nchini kwetu kutokuwapo," alisema.

Alibainisha kuwa Tanzania kwa kiasi kikubwa inaagiza mafuta hayo kutoka Malaysia ambako uzalishaji wake umepungua kutokana na kujifungia ndani kuhofia maambukizo ya corona.

"Kuanzia Julai 2020, mafuta yanayokuja nchini, yamesafishwa tayari. Kwa hiyo, viwanda vya kusafisha vile havifanyi kazi kama kawaida, wanafanya kazi wachache kuchukua tahadhari za corona.

Waziri huyo pia alisema kuna kero kwenye usafirishaji kwa kuwa wasafirishaji nao wanahangaika na tatizo la corona.

Alibainisha kuwa hadi sasa, zimefika meli mbili ambapo ya kwanza iliwasili Desemba 10 mwaka 2020 yenye shehena ya tani 21,800 na nyingine iliwasili Januari 5 mwaka huu.

"Hii ya kwanza tayari imeshakamilisha kupakua na mzigo upo sokoni tangu Januari 3 mwaka huu, hii ya pili inatarajiwa kuanza kupakua Januari 19, mwaka huu, lakini tunawasiliana na Waziri mwenzangu wa Uchukuzi ipangiwe kushusha mapema zaidi kama stoo zao zina nafasi ili kuingiza mafuta kwenye soko kwa uhakika," alisema.

Pamoja na hayo, waziri huyo alisema wizara imewekeza nguvu katika Mkoa wa Kigoma kupitia agizo la Waziri Mkuu kuhusu ushiriki wa taasisi za umma katika uzalishaji wa mchikichi kwa ajili ya usindikaji wa mafuta ya kula na kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vikubwa, vya kati na vidogo vya kusindika mbegu za mafuta, ili kutatua tatizo la uhaba wa mafuta ya kula nchini.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi (kulia), akiangalia korosho zilizovunwa kwenye shamba la Mkwese-Masigati, wilayani Manyoni, mkoani Singida katika ziara ya kikazi juzi. Kushoto ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manyoni, Charles Fussi. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

## Lukuvi apiga marufuku viongozi wa vijiji, vitongoji kuuza ardhi

**Na Munir Shemweta,** SINGIDA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amepiga marufuku viongozi wa vijiji na vitongoji nchini kujihusisha na uuzaji ardhi ikiwamo mashamba.

Amesema viongozi hao hawana mamlaka ya kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999.

Akizungumza wakati akikagua shamba la mikorosho la Mkwese-Masigati wilayani Manyoni mkoani Singida juzi, alisema viongozi wa wilaya na halmashauri wanapaswa kukomesha tabia ya baadhi ya viongozi wa vijiji na vitongoji kuuza ardhi kwa wananchi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, ugawaji ardhi kwenye vijiji lazima ufuate sheria iliyowekwa ikiwamo kuitisha mkutano na si kiongozi kujiamulia kugawa ardhi kwa niaba ya kijiji kizima.

"Kijiji kugawa ardhi lazima iwe kwenye mkutano siyo mtu anagawa. Mkuu wa Wilaya pita kote na elekeza mikutano ya kugawa ardhi isiitishwe kinyemela na wewe ukasimamie kujua wananchi watapata faida gani kwa ardhi itakayotolewa," alisema Lukuvi.

Waziri Lukuvi alisema mtu yeyote atakayenunua ardhi kwa mwenyekiti wa kijiji au kitongoji, ajue kuwa ni kinyume cha sheria kwa kuwa ardhi inatakiwa kuamuliwa katika mkutano.

Lukuvi aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni kwa uamuzi wa kugawa mashamba kwa ajili ya kilimo cha korosho na kueleza kuwa uamuzi huo unaifanya Manyoni kusonga mbele na kushauri kupewa muda ili kuona matokeo.

Aliitaka halmashauri hiyo kuhakikisha eneo la shamba la mikorosho, linapangwa kimji kwa kubuni mpango wa maendeleo na kufurahishwa na uamuzi wa halmashauri kuwa na mpango wa kumilikisha ekari 22,000 na kusisitiza kuwa wote watakaomilikishwa lazima wapatiwe hati za ardhi.

## ...Waliotelekeza hati za ardhi kupigwa faini

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imesema inaandaa utaratibu wa kuwatoza faini watu wote ambao watashindwa kwenda kuchukua kwa wakati hati miliki za mashamba na majengo, ili kupunguza mrundikano wa hati hizo katika ofisi za msajili wa hati.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Kamishna wa Ardhi Msaidizi, Shamimu Hoza, alipowasilisha mada kwenye mkutano wa Sekta ya Ardhi Mkoa wa Singida.

Shamimu alisema kulikuwa na tatizo katika uandaaji wa hati na watu kupata hati zao za umiliki baada ya kusubiri kwa muda mefu, lakini kwa sasa tatizo hilo limekwisha.

Alisema kuwa kwa sasa hati zinatengenezwa ndani ya muda mfupi, lakini wananchi hawaendi kuchukua hati zao.

"Kwa hiyo, kwenye masjala zetu za msajili wa hati unakuta tuna hati nyingi sana. Mkoa wa Singida hatuna hati nyingi sana kama mikoa mingine, lakini hata hizo chache tukiendelea kwa hali hii ya watu kusuasua kuchukua hati, ina maana zitakuwa nyingi," alisema.

Kwa mujibu wa kamishna huyo, utaratibu uliopo sasa ni kwamba kila Ijumaa wanazisambaza hati kwenye mitaa kupitia kwa watendaji wa mitaa na kuwajulisha kwa njia ya simu watu wote ambao hati zao zipo tayari, lakini pamoja na jitihada zote hizo, bado uchukuaji wa hati unasuasua.

Akifungua mkutano huo kwa niaba ya Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Anjelina Lutambi, Katibu Tawala Msaidizi (Utawala na Menejimenti ya Rasilimali Watu), Deogratius Yinza, alisema wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu mwaka jana, kilio kikubwa cha wananchi kilikuwa katika sekta ya ardhi.

## HABARI KITAIFA

# Sakata la mwalimu kubaka latua kwa DC

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

SAKATA la Mwalimu wa Shule ya Msingi ya Namibu B katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda mkoani Mara, kumbaka mwanafunzi wake, limeingia katika sura mpya baada ya wazazi kulalamika kwa Mkuu wa Wilaya.

Wazazi hao wamefikia hatua hiyo baada ya mtuhumiwa kukamatwa na kisha kupewa dhamana katika mazingira yanayodaiwa ni ya kutatanisha. Mtuhumiwa huyo anadaiwa kumbaka wanafunzi huyo ndani ya ofisi ya mwalimu mkuu wa shule hiyo.

Wazazi hao wanalalamikia uchunguzi wa vipimo alivyofanyiwa mtoto wao na daktari mmoja (jina tunalo) wa Hospitali ya Misheni Kibara na kujaza fomu namba tatu (PF-3) ya polisi kwamba hajabakwa huku mtoto mwenyewe akithibitisha kufanyiwa unyama huo.

Kutokana na hatua hiyo, wazazi wanadai kwamba kuna mazingira ya rushwa na sasa wameamua kwenda kwa Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, na kisha kutoa taarifa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani hapa, wakilalamikia kitendo hicho.

Mzazi wa mwanafunzi huyo, Lusia Kabuche, akiwa na mtoto wake huyo, juzi walifika ofisini kwa mkuu wa wilaya hiyo, kulalamikia kitendo hicho na kuomba msaada kutoka serikalini ili haki itendeke.

"Tumeamua kumuona mkuu wetu wa wilaya ili aweze kutusaidia maana daktari ameamua kupindisha ukweli. Lakini tumeamua kwenda TAKUKURU kutoa taarifa ili uchunguzi zaidi ufanyike maana tunasikia kwamba imetolewa milioni moja huyo mwalimu akadhaminiwa," alisema mmoja wa mzazi wa mwanafunzi huyo.

"Mtoto anasema amebakwa na mwalimu wake, lakini ushahidi unapindishwa. Hivi ni kweli mtoto wangu amsingizie mwalimu wake kwa kipi hasa? Kwani ana ugomvi naye mbona hatujawahi kusikia huo ugomvi? " Alihoji mzazi huyo na kuongeza kuwa:

"Tunaiomba serikali yetu inayoongozwa na rais wetu, mtetezi wa wanyonge, iingilie kati ili liwe fundisho kwa walimu na watu wengine wenye tabia kama hiyo maana tunawapatia watoto wetu ili wawafundishe wapate maarifa na siyo wawageuze kuwa wake zao."

"Kwa kitendo hicho hata kusoma hawezi kuwa makini kwa kumsikiliza mwalimu wakati wa masomo maana akimwona mwalimu huyo au mwalimu yeyote yule wa kiume atashtuka kwa hofu. Tunaomba msaada zaidi wa serikali," alisema.

Mwalimu Victor Magaji anatuhumiwa kwa kosa la kumbaka mwanafunzi wake (jina limehifadhiwa).

Inadaiwa kuwa siku hiyo, mwanafunzi huyo alikuwa akitoka kumsindikiza mama yake mzazi aliyekuwa anakwenda safarini na kwamba alipopita katika eneo la shule, ndipo mwalimu huyo alipomwita na kumwamuru aingie katika ofisi hiyo.

Pia inadaiwa kwamba baada ya mwanafunzi huyo kuingia ndani, mwalimu alifunga mlango na kumvua nguo kwa nguvu na kisha akaanza kumbaka huku akiwa amemziba mdomo kwa mikono yake na kumtaka asimwambie mtu yeyote vinginevyo atamuua.

Baada ya kufanyiwa ukatili huo, inadaiwa mwanafunzi huyo aliondoka eneo hilo na kwenda nyumbani kwao kisha akaamua kutoa siri hiyo kwa ndugu zake.

Kutokana na kutoa taarifa hizo, ndugu zake walimpeleka katika Hospitali ya Misheni ya Kibara kwa ajili ya uchunguzi na daktari aliyemfanyia uchunguzi anadaiwa kupindisha ukweli na kujaza fomu kwamba hajabakwa kitu ambacho kinalalamikiwa na wazazi wake, huku mtoto huyo akisisitiza kwamba amefanyiwa unyama huo.

Baada ya mwalimu huyo kukamatwa na askari wa kituo kidogo cha polisi Kibara, alipelekwa katika kituo kikuu cha polisi wilaya mjini Bunda na kupewa dhamana ambayo inalalamikiwa na wazazi kwamba kuna mazingira ya rushwa.

Mkuu wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, jana alipoulizwa kuhusu sakata hilo, alikiri kuwaona wazazi wa mwanafunzi huyo wakiwa na mtoto anayedaiwa kufanyiwa ukatili huo na kwamba wanafuatilia suala hilo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Daniel Shilla, jana, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kwamba uchunguzi unaendelea.

## Prof. Kanywanyi aagwa, azikwa Dar

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, jana, aliongoza umati uliokusanyika kuuaga mwili wa mwanasheria nguli nchini na mkongwe wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Prof. Josephat Kanywanyi (82), aliyefariki dunia Jumapili.

Tukio hilo lililofanyika jana asubuhi kwenye ukumbi wa Nkrumah wa UDSM, lilikusanya umati wa wasomi na wanasheria, wakiwamo mawaziri na majaji.

Miongoni mwa mawaziri waliohudhuria ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, aliyeambatana na Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma. Waziri Kabudi, ambaye miaka michache iliyopita, alikuwa mwanazuoni wa UDSM, aliwasilisha salamu maalum za majonzi kutoka kwa Rais John Magufuli.

Hadhira hiyo ambayo maziko yake yalifanyika katika makaburi ya Kinondoni, pia iliwakusanya Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, na wakongwe wa sheria UDSM, ambao sasa ni wastaafu akiwamo Prof. Issa Shivji na Dk. Ringo Tenga.

Ibada ya maziko ya msomi huyo ambaye pia amewafundisha wanasheria wengi nchini na nje ya nchi katika miaka yake 50 ya utumishi UDSM, iliongozwa na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Kanisa Katoliki Dar es Salaam, Thaddaeus Ruwa'ichi.Askofu Ruwa'ichi alimsifu Prof. Kanywanyi kwa mchango wake mkubwa nchini katika fani ya sheria na maboresho mbalimbali, sambamba na kanuni zake, akitaja baadhi ya maeneo yanahusu sekta za fedha na sheria ya bima katika kipindi cha mageuzi ya kiuchumi.



Dereva wa bodaboda akiwa amepakia wanafunzi kwa mtindo maarufu kama mshikaki katika eneo la Tegeta A, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Uhaba mafuta wapaisha bei samaki

**Na Christina Mwakangale**

KUPANDA kwa bei ya mafuta katika maeneo mbalimbali nchini kumesababisha kitoweo cha samaki kuuzwa kati ya Sh. 1,500 hadi 2,000 kwa fungu moja kutoka Sh. 1,000 hapo awali, katika Jiji la Dar es Salaam.

Nipashe ilitembelea maeneo tofauti ya jiji hilo, ambako huuzwa samaki waliokaangwa na kuuzwa kwa mafungu, ikiwamo Soko Kuu la Samaki la Kimataifa la Feri, Buguruni, Gongo la Mboto, Tegeta, na kukuta bei imepanda tofauti na wiki chache zilizopita.

Wakizungumza na Nipashe, mmoja wa wauzaji wa samaki hao, Musa Halfan, ambaye ni mkazi wa Mombasa alisema jana alinunua mafuta pamoja na samaki kwa bei ya juu, tofauti na wiki moja iliyopita.

Halfani alisema: "Jana nimekutana na kitu ambacho sikukitarajia, nimekuta samaki wanauza bei ya juu na mafuta pia. Imenibidi nami nipandishe bei, fungu moja la samaki waliokaangwa nauza kati ya Sh. 1,500 hadi 2,000 kulingana na aina," alisema Halfan.

"Ndoo ndogo ya mafuta ambayo yanatoka nje, inauzwa Sh. 80,000 kwa hiyo jana kama ningekuwa na mtaji wa kutosha ilipasa niwe na Sh. 160,000 kupata samaki na mafuta kwa ujazo unaolingana yaani kipimo cha ndoo ya lita 10," alisema Halfan.

Mkazi mwingine wa Buguruni, Mwanaisha Kombo, anayefanya biashara ya kuuza samaki waliokaangwa kwa zaidi ya miaka 10 alilieleza Nipashe kwamba kupanda kwa bei ya mafuta kumemlazimu naye apandishe bai ya samaki.

"Mafuta hayashikiki, wiki hii tangu ilipoanza nauza fungu la samaki kati ya Sh. 1,500 au 2,000 kutegemeana na aina, hii inatokana na mafuta ninayonunua kwa ujazo wa lita tatu kuuzwa Sh. 15,000," alisema Mwanaisha.

Kwa mujibu wa taarifa za Wizara ya Viwanda na Biashara, Tanzania hutumia Sh. bilioni 400 kwa ajili ya kuagiza mafuta ya kula.

Kadhalika, mahitaji ya mafuta hayo nchini ni tani 500,000 kwa mwaka, huku uwezo wa nchi kuzalisha mafuta ni tani 200,000.

# Ummy aonya NEMC kufanya kazi kipolisi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Ummy Mwalimu, amelitaka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuacha kufanya kazi kama polisi badala yake lishirikiane na wawekezaji.

Pia amelitaka baraza hilo kukaa na wawekezaji na kuwasaidia katika azma yao ya ujenzi wa viwanda badala ya kuwa kikwazo katika kutekeleza azma hiyo ya serikali.

Ummy alisema hayo juzi alipotembelea kiwanda cha BTY cha kurejeleza betri za magari kwa ajili ya kupata malighafi za kutengeneza betri na bidhaa zingine za plastiki, Buguruni jijini Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, Ummy aliambatana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Geoffrey, na uongozi wa NEMC ukiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Esnath Chaggu na Mkurugenzi Mkuu, Mhandisi Dk. Samuel Gwamaka.

Waziri Ummy alisema mwekezaji hakuandaa mpango wa usimamizi wa ardhi kulingana na bidhaa anazozitengeneza kama vile utiririshaji wa majitaka, vumbi wakati wa uzalishaji hali inayopelekea uchafuzi wa mazingira.

Kutokana na hali hiyo, Ummy aliagiza NEMC kukaa na mwekezaji kuangalia ni namna ya kuepuka madhara yanayotokana na uchafuzi wa mazingira na kwamba uwekezaji uende sambamba na kuhakikisha Sheria ya Mazingira inafuatwa ili kulinda afya za wananchi na mazingira kwa ujumla.

Alisema kiwanda cha BTY kinahitajika lakini ni lazima kizingatie mifumo ya usimamizi wa mazingira kwa sababu madini yanayotokana na urejelezwaji wa betri yana athari kwa mazingira na yanaweza kusababisha saratani na magonjwa mengine iwapo hakutakuwa na udhibiti endelevu katika usimamizi wa mazingira.

"Kiwanda kinalipa kodi za serikali na kimeajiri Watanzania wengi, lakini hiyo haitoshi kama hakizingatii sheria za mazingira zinasemaje katika uwekezaji," alisema.

Naye Waziri Mwambe alisema uwapo wa kiwanda cha BTY ni muhimu kwa sababu unasaidia kusafisha mazingira kwenye ukusanyaji wa betri mbovu kwa ajili ya kurejeleza, lakini uchakataji wake unafanyika katika hali ambayo si rafiki kwenye mazingira na hakijafuata taratibu za usimamizi wa mazingira kama inavyotakiwa.

"Kiwanda cha BTY kina faida hasa katika kupunguza takataka za betri kwenye mazingira yetu kwa sababu wanazikusanya na kuzirejeleza, lakini wanapaswa kuelekezwa namna bora ya utendaji kazi wao ili wasiharibu mazingira.

"Nchi yetu inahitaji viwanda vingi ili viendelee kutoa ajira kwa vijana wetu na pato letu la taifa liongezeke kwa sababu wanalipa kodi. Pamoja na hayo, suala la utunzaji wa mazingira ni lazima lifuatwe kwa faida ya kizazi hiki na kijacho," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Gwamaka, alisema wamiliki wa viwanda Tanzania wajitahidi kupata wataalamu elekezi wa mazingira wenye uwezo wa kuwasaidia kuwashauri vizuri kuhusu mazingira wakati wa uwekezaji.

Aliwataka wawekezaji hao kufika NEMC pale wanapopata changamoto za kupata wataalamu elekezi wa mazingira ili kuepuka kufungiwa au kutozwa faini.



Ofisa Misitu na Uhifadhi Mazingira wa Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Kanda ya Kusini, Kelvin Lilai, akiwaonyesha wananchi wa Kijiji cha Mijelejele, jinsi ya kupanda miti ya mitiki kwa kuzingatia kanuni za upandaji miti, wakati wa uzinduzi wa kampeni ya upandaji miti kijijini hapo, wilayani Masasi, mkoani Mtwara jana, zaidi ya miti 6,000 inatarajiwa kupandwa. **PICHA: HAMISI NASRI**

## Mauzo madini Kahama yapaa

**Na Mohab Dominick**, KAHAMA

MAUZO ya dhahabu katika soko la Mwime, wilayani Kahama, yameongezeka kutoka gramu 167 kwa mwezi hadi kilo moja, imefahamika.

Hatua hiyo inatokana na Waziri wa Madini, Dotto Biteko, kufanya ziara katika soko hilo na kubaini utoshaji wa madini hayo, hivyo kuwawajibisha wahusika ikiwamo kusimamishwa kazi kwa mwenyekiti wa soko, Samuel Nalimi.

Katika ziara hiyo, watuhumiwa 11 wa utoroshaji wa dhahabu ambao ni wanunuzi, walikamatwa na kufikishwa katika vyombo vya sheria.

Mwenyekiti mpya wa soko hilo, Bahati Makaya, alisema juzi kwamba kwa sasa ununuzi wa madini hayo umeongezeka kutokana na hatua zilizochukuliwa pamoja na udhibiti.

Makaya ambaye ni dalali katika soko hilo, alisema tukio la kukamatwa watoroshaji hao lilitokea baada ya Waziri wa Madini kufanya ziara katika soko hilo na kubaini madudu yalikokuwa yakifanyika ikiwamo utoroshaji wa madini.

Alisema baada ya kukamatwa kwa watuhumiwa hao, mauzo ya dhahabu katika soko hilo yamepanda kutoka gramu 167 kwa mwezi hadi kilo moja hali ambayo inaleta matumaini makubwa ya kupanda kwa mauzo.

Makaya alisema kwa sasa ofisi ya madini haina budi kuongeza watumishi katika machimbo ya Mwime Ilindi, ili kutoa elimu ya madini hali ambayo itatoa uelewa mkubwa kwa wamiliki.

Kuhusu hali ya miundombinu katika soko hilo, alisema hali ya barabara zinazokwenda katika machimbo hayo ni mbovu na zinahitaaji matengenezo makubwa na kuongeza kuwa wachimbaji wamekuwa wakilipa tozo nyingi kwa halmashauri, lakini hali hiyo bado si nzuri.

"Tunaomba halmashauri ielekeze nguvu zake katika kutengeneza miundombinu ya barabara za kuingia katika machimbo kwani tunachangia tozo mbalimbali za serikali," alisema.

Mwenyekiti huyo alimpongeza Rais John Magufuli na Waziri wa Madini, Biteko, kwa kuwathamini wachimbaji wadogo tofauti na ilivyokuwa katika kipindi cha nyuma kwa kuwa walikuwa wakigundua madini na baadaye kunyang'anywa maeneo na watu wenye fedha.

# Wagoma kuhamishwa eneo la kimondo

**Na Thobias Mwanakatwe**

ZAIDI ya wakazi 600 wa kitongoji cha Isela, Kijiji cha Ndolezi wilayani Mbozi, wameingia katika mvutano mkali na serikali baada ya kutakiwa kuhamishwa kupisha Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) kuchukua eneo hilo, ili kukiboresha kivutio cha utalii cha kimondo kilichoko kijijini hapo.

Mpango huo wa NCAA una lengo la kutwaa ardhi hiyo yenye ukubwa wa ekari 600 na kuhamisha zaidi ya kaya 200, ili kukitanua kituo kimondo na kuwa hifadhi ndogo kwa kuongezea wanyama watakaohamishiwa hapo kutoka mamlaka hiyo.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mbunge wa Vwawa, Japhet Hasunga, na kuhudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, John Palingo na Kamati ya Ulinzi na Usalama pamoja na viongozi wa NCAA, wananchi hao walishikilia msimamo wa kutoondoka kwa madai uhamishaji huo unafanyika kibabe bila kuwashirikisha na kuwapatia elimu.

Wananchi hao walilalamikia hatua ya Jeshi la Polisi kufika katika kitongoji hicho na kutumia nguvu kwa kurusha mabomu ya machozi kwa lengo la kuwatisha baada ya kikao cha awali kuvurugika kutokana na kugoma kutia saini fomu za kuridhia kufidiwa.

Katika mkutano huo, zaidi ya wananchi 20 wakiongozwa na kiongozi wao wa kimila, Chifu Mtazi Mwamengo, walieleza sababu kadhaa zinazofanya wasiwe tayari kuachia eneo lao, ikiwamo kutopewa elimu ya kutosha wala kuambiwa wapi watapelekwa baada ya kutolewa hapo.

Chifu Mwamengo alisema yeye yuko upande wa wananchi kwa kuwa hawakupewa elimu ya kutosha juu ya kuondolewa kwao, lakini ni wapi watapelekwa licha ya kupewa fidia.

Mmoja wa wananchi hao, Junes Kayala, alisema baada ya kuonyesha msimamo wake wa kugoma kutia saini fomu hizo za Ngorongoro, amenyimwa mgawo wa fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF),

Katika hali isiyo ya kawaida, Kayala baada ya kumaliza kutoa malalamiko hayo mbele ya mbunge, ghafla alidondoka chini na kuangua kilio kikali huku akiungwa mkono na baadhi ya wanawake waliokuwa kwenye eneo la mkutano na kumlazimu mbunge na viongozi wengine kutumia nguvu ya ziada kuwatuliza.

Baada ya kuwasikiliza wananchi hao, Hasunga aliitaka NCAA kusitisha mpango huo na kuanzisha mchakato upya wa kutoa elimu, ikiwamo kuangalia njia nyingine itakayowezesha kuliendeleza eneo hilo ili liendelee kuleta manufaa kwa jamii na wananchi.

Naye Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Stan Mwamsojo, alisema uhamishaji huo unakwenda kinyume cha ilani ya chama hicho inayotaka wananchi walio karibu na maeneo ya uwekezaji wawe wanufaika wa kwanza.

Naibu Kamishna wa Uhifadhi wa NCAA, Dk. Christopher Timbuka, alisema amepokea ushauri wa mbunge wa kuanza upya mchakato ili pande zote kuwa na uelewa mmoja.

# Tanzania, China zazindua programu kuongeza watalii

**Na Elizabeth Zaya**

TANZANIA na China zimezindua programu ya kutangaza utalii kwa kutumia kadi maalum (Post Cards), lengo kuu ni kuongeza idadi ya watalii.

Akizungumza wakati wa kusaini makubaliano ya kuendesha programu hiyo jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Jaji mstaafu, Thomas Mihayo, alisema lengo ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2025, idadi ya watalii watakaofika nchini iwe milioni tano.

Alisema katika programu hiyo watashirikiana na kampuni 17 kutoka China zinazojihusisha na usafirishaji watalii wa ngazi za juu.

Jaji Mihayo alisema: "Programu hii pia inaashiria kuonyesha upendo na kujali watu, katika kipindi cha mwaka 2020 ambacho Wachina hawajasafiri nje ya nchi yao kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona."

Aliongeza: "Tunaamini kwamba 'post cards' hizi zitaleta matumaini mapya hususani kwa mwaka mpya wa Kichina, kwamba utakuwa ni wa baraka na watasafiri nje ya nchi yao."

Zaidi Jaji Mihayo alisema: "Na upongeza ubalozi wa Tanzania nchini China kwa juhudi wanazoendelea nazo za kuvumbua mbinu mbalimbali za kutangaza utalii wa nchi yetu, huu ni mfano wa kuigwa na balozi zingine, jumuiya na taasisi pia."

Naye Mwakilishi wa Balozi wa China nchini, Wang Siping, alisema pamoja na kutokea kwa mlipuko wa ugonjwa wa corona duniani kulikowazuia Wachina kusafiri, wanaamini mwaka huu utakuwa na matumaini mapya kwa watalii kutoka katika nchi hiyo kuja Tanzania.

"Na tunaamini kwamba kupitia kadi hizi maalum zitasaidia kutangaza kwa kiwango kikubwa utalii wa Tanzania katika soko la China, tuna idadi kubwa ya watu ambao wameonyesha kuvutiwa kuitembelea baada ya dunia kurudi katika hali yake ya kawaida," alisema Siping na kuongeza:

"Na tunaamini kwamba Wachina watafurahia kuona uzuri wa Tanzania, hivyo kuwavutia watu wengi zaidi kuitembelea nchi hiyo."

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zinaibuka kwa kasi katika kuwavutia watalii kutoka katika nchi mbalimbali duniani, kwamba kupitia programu hiyo italeta mafanikio makubwa katika sekta ya utalii.

# Waziri: Wawekezaji wadaiwa katika ranchi wanyang'anywe

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameiagiza Bodi ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kuwanyang'anya wawekezaji ranchi zote walizokodishwa na kushindwa kulipa madeni.

Ndaki alitoa maagizo hayo jana, akiwa wilayani Mbarali mkoani Mbeya wakati akizungumza na wakulima na wafugaji katika Bonde la Usangu.

Alisema serikali inahitaji ranchi zote zilipe madeni kuanzia Januari 12 hadi Februari 15, mwaka huu na kwamba zitakazoshindwa kulipa, zinyang'anywe na kupewa wawekezaji wengine.

Pia alipiga marufuku kufanyika kwa shughuli za kilimo kwenye maeneo ya ranchi kwa madai kuwa ni kwenda kinyume cha makubaliano ya mkataba.

"Nimetoa muda wa kuanzia Januari 12 hadi Februari 15 majira ya saa saba mchana, Bodi ya NARCO iwe imekusanya madeni yote wanayoyadai kwenye ranchi mbalimbali nchini, lakini pia wawekezaji kufuata makubaliano ya mikataba ili kila upande unufaike na ranchi hizo," alisema.

Katika hatua nyingine, Ndaki aliwahakikishia wawekezaji katika wa ranchi mbalimbali nchini kwamba serikali imewaandalia mazingira mazuri ya kufanya shughuli zao na kuomba waendelee kushirikiana.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Elisaante ole Gabriel, aliwaomba wamiliki wa ranchi kutumia maeneo hayo kwa ajili ya mifugo tu na shughuli zingine ambazo ni kinyume cha makubaliano.

Baadhi ya wakulima wa Bonde la Usangu walioomba serikali kuwagawia eneo kwa ajili ya kilimo kuliko ilivyo sasa ambapo wanakodishwa kwa gharama kubwa.

Ulia Mahenge aliiomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvivu kupewa eneo kwa ajili ya kilimo na kwamba yuko tayari kulipia gharama za vitalu.

Juzi, Mwekezaji wa Ranchi ya Usangu, Basil Mramba, alimhakikishia Waziri Ndaki, kulipa madeni yote ndani ya muda uliopangwa.

Alipongeza hatua ya Waziri Ndaki kutembelea eneo lake ambalo lina ukubwa wa hekta 43,727, huku wakimiliki ng'ombe 531 na kwamba tayari walikwishaanza kulipa deni tangu awali ambapo ng'ombe 100 waliuzwa.



Katibu Mwenezi na Itikadi wa CCM ambaye ni Mbunge wa kuteuliwa na Rais, Humphrey Polepole, akizungumza na wananchi mbalimbali wa Mkoa wa Dar es Salaam, wakati akisikiliza kero zao katika Mtaa wa Lumumba, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwambe aitaka TBS kupunguza muda kuandaa viwango na usajili

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, amelitaka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kupunguza muda wa kuandaa viwango kutoka miezi tisa hadi mitatu na muda wa usajili wa bidhaa na kutoa alama ya ubora kutoka miezi mitatu hadi mmoja.

Amesema hatua hiyo itawarahisishia wajasiriamali kufanya na kukuza biashara zao kwa urahisi.

Akizungumza juzi alipofanya ziara katika shirika hilo, alisema muda uliowekwa na TBS katika kuandaa viwando na kusajili alama ni mrefu na unakwamisha wafanyabiashara na nchi kwa ujumla. Pia alitembelea na kufanya mazungumzo na menejimenti ya Wakala wa Vipimo (WMA).

Waziri Mwambe aliliagiza shirika hilo kufanya ukaguzi wa bidhaa kwa kushirikiana na taasisi zingine zinazohusika na ukaguzi wa mizigo bandarini na mipakani ili kupunguza muda unatumika kukagua bidhaa hizo, kupunguza mianya ya rushwa na kurahisisha utoaji wa mizigo hiyo kwa haraka.

Sambamba na hilo, alihimiza TBS kufanya kazi kwa karibu na maofisa biashara wa halmashauri ili kurahisisha utoaji wa elimu na usimamizi wa viwango kwa wajasiriamali, ili kupanua uwigo wa utoaji huduma na kuwafikia wajasiriamali wengi walioko katika halmashauri hizo.

Aidha, aliielekeza TBS kufanya kazi kwa pamoja na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) katika kuandaa viwango na miongozo yenye vigezo rahisi vitakavyowawezesha wajasiriamali kuanzisha viwanda vidogo ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa, kukuza biashara kuongeza ajira na pato la taifa.

Naye Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alizitaka TBS na Wakala wa Vipimo (WMA) kuhakikisha zinasimamia viwango na ubora na vipimo sahihi vya bidhaa za Tanzania ili kuziwezesha kuingia katika soko la ushindani ndani na nje ya nchi.

Aidha, aliziagiza taasisi hizo kuendelea kuimarisha ukaguzi wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi zinakuwa na viwango na vipimo sahihi ili kuiepusha Tanzania kuwa dampo la bidhaa hafifu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hili la ujenzi holela ni muhimu kuangaliwa

**TATIZO** la ujenzi holela limeonekana kuwa sugu nchini kutokana na kutofuatwa utaratibu wa mipango miji na baadhi ya watu kujijengea nyumba ovyo.

Ujenzi holela husababisha miundombinu muhimu kushindwa kupitishwa katika baadhi ya maeneo kwa sababu ya kukosa njia za kupita.

Inapotokea majanga makubwa kama ya moto, mafuriko uokoaji hushindwa kutekelezwa kwa wakati kutokana na kukwama kufika eneo husika kwa kukosa barabara.

Tatizo hili la ujenzi holela chanzo kikubwa ni baadhi ya watu kununua ardhi kienyeji kwa kukatiwa vipande bila kujali mpangalio wa kuwezesha miundombinu ya barabara, umeme na maji kupitishwa maeneo yanayohusika.

Ujenzi holela pia umechangia maeneo mengi ya miji kukumbwa na mafuriko kwa sababu njia zinazotakiwa kupita maji hayo kuzuiwa na ujenzi.

Juzi Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, akiwa katika ziara yake mkoani Singida, aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri nchini kusimamia ardhi kuanzia ngazi za mitaa na vijiji ili ziweze kuepuka na ujenzi holela na kurahisisha ufuatiliaji makusanyo ya kodi ya pango la ardhi.

Akitoa agizo hilo Lukuvi alisema ni vyema wakurugenzi katika halmashauri nchini wakawapa wajibu watendaji wa mitaa na vijiji kwa barua kusimamia misingi ya ardhi yenye lengo la kusimamia sheria katika masuala ya ardhi.

Hata hivyo, akatoa tahadhari kuwa watendaji wa mitaa na vijiji watakaokasimia mamlaka ya usimamizi ardhi katika maeneo yao hawatakuwa na jukumu la kugawa, kupanga, kupima na kumilikisha ardhi, bali kuangalia yanayoendelea katika mitaa yao na wakikuta ukiukwaji wowote wa ujenzi holela watakuwa na wajibu wa kusitisha.

Ufafanuzi huo umeweka wazi mipaka ya watendaji hao katika kusimamia suala la ardhi katika vijiji na mitaa yao.

Ni jambo jema kwa watendaji wa mitaa kuzungukia maeneo yao na kusitisha ujenzi holela ambao husababisha kero na migogoro kwa wakazi kwa sababu mtu ameamua kuziba njia kwa kujenga ukuta kuzunguka nyumba yake bila kujali wenzake watapita wapi.

Waziri Lukuvi katika agizo hilo amewataka watendaji hao kutengeneza majedwali maalum yenye orodha inayoonyesha kila mmiliki wa kiwanja kwa lengo la kuwawezesha watendaji wa mitaa kuwajua katika maeneo yao.

"Kumbukumbu zote za masuala ya ardhi wajulishwe watendaji wa mitaa na vijiji ili waweze kufuatilia katika mitaa yao," alisema Lukuvi.


Ofisi za ardhi za mikoa pia zimetakiwa kutoa elimu kwa watendaji wa mitaa na vijiji ili kuwajengea ufahamu wa masuala ya ardhi na kuwawezesha kusimamia vyema masuala hayo katika maeneo yao.

Kwa mujibu wa Lukuvi, hata kama manispaa imepanga matumizi bora ya ardhi ni vyema matumizi yake yakawekwa kwenye vipande vya ngazi ya mitaa na kuwa kazi hiyo ni ya halmashauri kwa kuwa mitaa ni jicho lake la kutoa taarifa katika masuala mbalimbali yakiwamo ya ardhi.

Halmashauri zote zimepewa wajibu wa kusimamia ardhi katika maeneo yao na ilichofanya Wizara ya Ardhi ni kuwapatia wataalamu watakaowasaidia kujua namna bora ya kutumia ardhi vizuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Sasa ushindi jimboni uviondoe viti maalum

**BUNGE** ndilo linalohusika na maamuzi muhimu yahusuyo nchi kuanzia kutunga sheria, bajeti za serikali, sera, mipango na mambo mengine muhimu kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Wanaoingia bungeni hupatikana kwa njia tatu, mosi kuchaguliwa majimboni kwenye kura, wanawake wanaoingia kupitia viti maalumu na 10 wanaoteuliwa na rais.

Hata hivyo, kwa muda mrefu, wanawake wamekuwa wakipiga kelele wakitamani kuwapo kwa uwiano kati yao na wanaume, katika nafasi za uongozi ukiwamo ubunge wa majimboni badala ya viti maalumu.

Kilio chao kinatokana na ukweli kwamba, tangu nchi ipate uhuru, ushiriki wa wanawake katika bunge haujafikia asilimia 50 kwa 50 kwa kuchaguliwa majimboni, ambayo wamekuwa wakiitamani.

Ili kufanikisha lengo lao hilo, wamekuwa wakihamasishwa kuwania nafasi za uongozi, kwa kuwa wanayo fursa katika kukuza hata uchumi wa nchi.

Kwa mfano, kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana, kulikuwapo na majukwaa mbalimbali ya kuhamasisha wajitose kuwania ubunge kwenye majimbo mbalimbali na udiwani katika uchaguzi.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ulifikia kuandaa ilani ya uchaguzi ya wanawake na kuisambaza katika vyama mbalimbali vya siasa, ili viwateue kuwania urais, ubunge na udiwani.

Ilani hiyo ya kuendeleza madai ya wanawake watetezi wa haki za ushiriki katika uongozi wa kisiasa, ilibeba madai yao, kwa kuwa ni wadau na washiriki wakuu katika michakato mbalimbali ya uchaguzi.

Pamoja na juhudi zao hizo, hakujawa na la kujivunia bado asilimia 50 kwa 50 hasa kwenye ubunge haijafikiwa ni kutokana na ukweli kwamba, katika uchaguzi mkuu uliopita ni wanawake wachache wamepata ubunge wa majimbo.

Katika majimbo zaidi ya 250 ya uchaguzi, wanawake walipata ubunge wa majimbo hawazidi 20, hali inayoonyesha kuwa bado wana safari ndefu ya kufikia malengo yao wanayotamani.

Ipo mikoa mingi ambayo haina wabunge wanawake wa majimbo kama Mara wenye majimbo 10, ambayo yote yana wabunge wanaume, kana kwamba hakukuwa na wanawake waliojitokeza. Umefika wakati sasa wa wanawake kujiuliza wanakwama wapi na hadi lini wasifikie kile wanachokitamani? Je, ni mfumo dume au ni vyama vyao kutokuwaamini au kuna sababu nyingine wanazozijua, zinazokwamisha?

Kwa kauli zao kuna wakati wanasema wamechoka kuwa wabunge ama madiwani wa viti maalum na wanatamani kuchaguliwa majimboni na kata, lakini wameendelea kushinda wachache.

Wakati mwingine mila na utamaduni hasa mfumo dume, fedha za kugharamia uchaguzi, utekelezaji mdogo wa sera za kimataifa na kitaifa kuhusu usawa wa kijinsia na vyama kutowapa nafasi huenda vikawa vikwazo kwao.

Ubunge kupitia majimbo ni wa muhimu, katika baadhi ya vyombo vya serikali ambavyo vinashughulika na kuandaa sera na mipango ya maendeleo, kwa kuwa wana uwezo kama walivyo wanaume.

Wanawake ndiyo wapigakura wakuu, wanatambua kuwa ni wadau muhimu katika shughuli zote za kisiasa na maendeleo ya jamii, wasikate tamaa, badala yake waendelee kupaza sauti ya kudai asilimia wanazotaka.

Lakini pamoja na hayo, suala ya kukaa na kutafakari ni wapi wamekosea, ni la muhimu, kwa kuwa litawasaidia kuibuka na mikakati zaidi ya kufanikisha ajenda yao ya kutaka asilimia 50 kwa 50 ifikapo 2025.

Yawezekana mfumo dume, unachangia kutokuwapo kwa usawa katika uwiano wa wanawake na wanaume kwenye uwanja wa siasa, hasa wakati huu wa mfumo wa vyama vingi vya siasa hivyo wajitahidi kupitia majukwaa yao kupambana na utamaduni huo unaowakwamisha.

# SHEREHE ZA MAADHIMISHO MIAKA 57 YA MAPINDUZI ZANZIBAR




Askari wa Vikosi vya Ulinzi wakipita na vifaru wakati wa maadhimisho hayo. **PICHA: OMR**



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, akijadiliana jambo na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad, katika maadhimisho ya miaka 57 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. **PICHA: OMR**



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (kushoto), akisalimiana na Rais mstaafu Mzee Ali Hassan Mwinyi, baada ya kuwasili katika kilele cha maadhimisho ya miaka 57 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika viwanja vya Mnazi Mmoja jana. Wa (pili kushoto) ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla na Rais mstaafu wa Zanzibar, Amani Abeid Karume. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**



Magari maalum ya Jeshi la Polisi yakipita katika maadhimisho hayo. **PICHA: OMR**




Wafanyabiashara wadogo wakiwa na bango la kumpongeza Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati wa maandamano ya maadhimisho hayo. **PICHA: OMR**



Wanachama wa vyama mbalimbali vya siasa wakiwa katika maadhimisho hayo. **PICHA: OMR**

# TRC yatakiwa kudhibiti upotevu mapato

**Na Tiganya Vincent,** TABORA

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC) limetakiwa kutoa mafunzo kwa watumishi wake, ili kusimamia vyema mapato kwa ajili ya kuliwezesha kujiendesha kwa faida bila kutegemea fedha kutoka serikalini.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alisema hayo juzi, wakati wa ziara yake ya kukagua miundombinu ya TRC na Chuo cha Reli Tabora.

Alisema TRC inatakiwa kutengeneza mfumo wa kisasa na kuachana na mfumo wa kizamani wa ukusanyaji mapato kwa njia ya mkono ambao unaruhusu upotevu wa fedha za umma kwa kuwa hautoi taarifa sahihi ya fedha zilizokusanywa katika vituo husika na vile vya njiani.

Kasekenya alisema serikali imewekeza fedha nyingi katika ujenzi wa miundombinu ya reli, hivyo ni lazima shirika hilo lihakikishe linakuwa na wataalamu wazalendo na waadilifu ambao watakuwa tayari kufanya kazi kwa maslahi ya nchi na kwa kutumia mfumo wa kisasa wa ukusanyaji mapato ambao unatoa uwazi.

Naibu Waziri aliagiza wataalamu wa chuo cha reli kuhakikisha wanawasaidia watumishi wa shirika kutengeneza mfumo ambao utawezesha mapato yote yanayopatikana kwenda sehemu husika na si kuishia mifukoni mwa watu wasio waadilifu.

Kasakenya alisema fedha nyingi zinazotokana na usafirishaji wa abiria na mizigo, zinapotea na kuishia mifuko kwa watu wachache kwa sababu ya kutumia mfumo wa zamani wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya mikono.

"Unaweza kukuta msafiri amepandia hapa Tabora Mjini na anakwenda Kigoma, lakini nauli atakayetozwa ni ya kuanzia Kazulamimba huko ya kuanzia Tabora hadi Kazulamimba haijulikani. Lazima mje na suluhisho la tatizo hili ambalo limechangia kudhoofisha shirika.

Shirika hili ni lazima lifanye kazi kwa ufanisi ili kujiendesha na lisaidie katika kuokoa barabara zinazojengwa kwa kuchukua jukumu la kusafirisha mizigo mizito ambayo ikipita katika barabara zetu, inasababisha zisidumu kwa muda mrefu," alisisitiza.

Kasekenya pia aliwataka watendaji wakuu wa wilaya Tabora kufanya safari za kushtukiza katika njia za reli ya kwenda Tabora, Mpanda, Mwanza na Dodoma ili kujionea hali halisi ya mapato yanayokusanywa kutoka kwa abiria na mizigo ya vituo vya njiani.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuwabana watumishi wa magari ya abiria na yale ya mizigo ambao si waaminifu kuchukua abiria na mizigo ya njiani na fedha kuweka mifukoni mwao.

Katika hatua nyingine, Kasekenya aliwataka wananchi wanaoishi kandokando ya miundombinu ya reli na barabara kuwa walinzi ili kuhakikisha inadumu kwa muda mrefu na kuleta tija kwa wananchi wengi.

Kasekenya alisema uharibifu wa miundombinu ya teli na barabara umekuwa ukisababisha Taifa hasara kubwa na kurudisha nyuma maendeleo ya jamii inayozunguka maeneo hayo.



Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu, Wakala wa Maabara ya Veterinari (TVLA), Dk. Stella Bitanyi (kulia), akifafanua jambo kwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul (katikati), alipotembelea kituo cha wakala hiyo wilayani Kibaha, mkoani Pwani juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfanyabiashara kutozwa 50,000/- kwa uchafu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MWENYEKITI wa Soko la Mnarani, maarufu kama Loliondo, lililoko katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Mohamed Mnembwe, amesema mfanyabiashara atakayebainika eneo lake kuwa chafu, atatozwa faini ya Sh. 50,000.

Akizungumza na waandishi wa habari sokoni hapo jana, Mnembwe alisema faini hiyo ni moja ya kanuni za soko hilo zilizowekwa kuimarisha usafi wa mazingira kwa wafanyabiashara na wateja.

Mnembwe alisema lengo la kuweka faini hizo ni kupambana na magonjwa ya mlipuko ambayo yakitokea, shughuli zote za kijamii zitasimama ikiwamo biashara na kurudi nyuma kiuchumi.

"Kila mfanyabiashara anatakiwa kuwa msafi kwenye eneo lake la biashara na kuhakikisha takataka zinahifadhiwa katika sehemu maalumu zilizotengwa sokoni kwani hapa kuna vitu vingi vinauzwa vya kula, hivyo usafi unatakiwa kuwa wa hali ya juu na ni wajibu wa kila mmoja kuzingatia hili," alisema.

Mnembwe alisema mfanyabiashara atakayetozwa faini na kukaidi kulipa anaweza kupata adhabu ya kuondolewa sokoni kuendelea na biashara katika eneo hilo kwa kwenda kinyume cha kanuni zilizowekwa.

Mwenyekiti huyo alisema wako pia mgambo katika soko hilo ambao moja ya kazi yao ni kusimamia usafi na kuwabana wafanyabiashara ambao wanatupa taka ovyo.

Kuhusu mitaro iliyoko sokoni hapo, Mnembwe alisema uongozi wa soko umeomba halmashauri kufunika mitaro kwa usalama wa wafanyabiashara na wanunuzi wa bidhaa katika soko hilo.

Hata hivyo, alisema katika upande wa ukusanyaji taka wanakabiliwa na kikwazo cha gari kutopita kwa wakati kukusanya taka, hivyo kusababisha baadhi ya maeneo taka kuzagaa ovyo na kusababisha hofu ya magonjwa ya mlipuko hususani katika kipindi hiki cha mvua.

# Mtaaluma alia na utoro wanafunzi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWALIMU wa Taaluma katika Shule ya Sekondari Ulayasi wilayani Ludewa, Timoth Haule, amelalamikia utoro kwa wanafunzi wa kiume takribani 27 wa kidato cha kwanza hadi cha nne ambao wamepangiwa na wazazi wao mitaani kutokana na kukosa bweni.

Pia mwalimu huyo ameelezea uhaba wa walimu wa Hisabati na Fizikia, huku akibainisha kuwa mwalimu wa Fizikia aliyepo anafundisha kidato cha kwanza hadi cha sita.

Haule aliyasema hayo juzi katika kikao cha walimu, mbunge wa jimbo hilo na kubainisha kuwa utoro wa wanafunzi hao unasababishwa na wazazi kuwapangia nyumba mitaani.

"Kwa sababu hakuna bweni la wanafunzi wavulana, wamepangiwa nyumba mitaani. Kwa sababu huko mitaani wanakaa wengi, wanamtuma labda mwanafunzi mmoja aje aangalie nini kinaendelea shuleni. Hali hii si nzuri hata kidogo kwa sababu wakati wa kufundisha, wanafunzi wa kiume wanakuwa hawapo," alisema Haule.

Pia alisema wakiona wanafunzi hawajatokea kabisa, hulazimika kwenda kuwawinda mitaani ili kuwaleta shuleni.

"Tunalazimika kuwawinda kuwarudisha shuleni ili waingie darasani. Sasa hii inatupatia shida kwa sababu tunaacha vipindi kwenda kuwatafuta watoto kwa kuwa nusu ya darasa liko nje. Wazazi nao kama wamewatupa watoto wao," alisema Haule.

Mbunge wa Ludewa, Joseph Kamonga, alisema suala la kuwinda wanafunzi si la walimu, hivyo linapaswa kufuatiliwa na kamati ya maendeleo ya kata.

"Si kazi ya mwalimu kugeuka mgambo kwa kufukuza wanafunzi anaweza hata akauawa, hii ni kazi ya kamaka kuitisha kikao kujadili hili na mimi nitashiriki, kazi ya mwalimu ni kufundisha si kukimbiza watoto," alisema Kamonga.

Naye mmoja wa wanafunzi, Gladness Kilonge, alisema licha ya changamoto shuleni hapo wanaomba kuongezewa mwalimu wa Fizikia kwani aliyepo amezidiwa kutokana na kufundisha kidato cha kwanza hadi cha sita.

**Licha ya changamoto shuleni hapo wanaomba kuongezewa mwalimu wa Fizikia kwani aliyepo amezidiwa kutokana na kufundisha kidato cha kwanza hadi cha sita.**

## Halmashauri yatamba kukamilisha madarasa

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

HALMASHAURI ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, imesema itakamilisha ujenzi wa madarasa yanayohitajika kwa ajili ya wanafunzi waliofaulu kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza mwaka huu katika muda uliopangwa.

Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Jumanne Mwankoo, alisema hayo juzi wakati akitoa taarifa ya ujenzi huo kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri Wilaya (DCC) kilichofanyika kwenye ukumbi wa Cluster ya Walimu wa Tarafa ya Mlingoti mjini hapa.

Alisema halmashauri imejipanga kuhakikisha ujenzi huo unakamilika kabla ya muda uliopangwa na serikali ili wakati shule zitakapokuwa zinafunguliwa, watoto wote waliofaulu kuanza masomo ya sekondari.

Mwankoo alisema mwaka huu halmashauri yake ilikuwa na upungufu wa vyumba vya 15 kutokana na kufanya maandalizi makubwa mwaka 2019/20 ambapo walijenga zaidi ya vyumba vya madarasa 40.

Alisema awali halmashauri ilijipanga kukamilisha idadi hiyo kabla ya muda uliopangwa na serikali ili wakati shule zitakapokuwa zinafunguliwa, watoto wote waliofaulu kujiunga na masomo ya sekondari mara moja.

Mwankoo alisema tayari halmashauri imekwishapeleka Sh. milioni 157 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa na ukamilishaji wa ofisi na madarasa ambayo ujenzi wake ulianza mwaka jana.

Hata hivyo, alisema ujenzi huo unakabiliwa na ukosefu wa saruji, lakini unaendelea katika Shule ya Sekondari Muhuwesi ambako shule imeazima saruji kutoka shule nyingine ambayo ilinunua kabla bidhaa hiyo haijaadimika.

Alisema eneo lingine ambako ujenzi unaendelea kwa sasa ni katika shule tarajali za sekondari za kata za Mindu na Misechela ambako wanaendelea na ujenzi wa madarasa matano kila shule kwa kufanya shughuli ambazo hazihitaji saruji na ukamirishaji utaendelea kwa kupiga plasta baada ya kupata saruji.

Ili kupunguza gharama za ujenzi huo, alisema tayari wameagiza mifuko 1,200 ya saruji kutoka kampuni ya Dangote pamoja na kuagiza mabati bando 84 sawa na mabati 1,008 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi huo.

Kuhusu madawati, alisema halmashauri inaendelea na utengenezaji wa seti 542 za viti na meza vilivyogharimu Sh. milioni 29 kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi hao wanaotarajia kujiunga na kidato cha kwanza.

# Waziri aiagiza WMA ukaguzi wa kushtukiza

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, ameutaka Wakala wa Vipimo (WMA) kufanya ukaguzi wa kushtukiza wa mara kwa mara ili kuwabaini wafanyabiashara wanaopunja vipimo.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam juzi, alipofanya ziara kwenye ofisi za (WMA) zilizoko Ilala kwa ajili ya kujionea shughuli zinazofanywa na wakala na kuzungumza na wafanyakazi.

Mwambe alisema amebaini changamoto kwenye viwanda kwa kuwa baadhi ya wazalishaji ambao si waaminifu, wamekuwa wakifungasha bidhaa pungufu kinyume na ilivyoandikwa kwenye vifungashio.

Alisema hata kwenye uzalishaji wa nondo kumekuwa na changamoto ya kusema ukweli kwa kuwa wengi wamekuwa wakiweka vipimo ambavyo si sahihi na kuwaibia wateja.

**Kuna umuhimu kwa WMA kuwa na majengo yake na kuachana na utaratibu wa kupanga hali inayosababisha kutumia fedha nyingi kulipia majengo hayo.**

"Wako wafanyabiashara ambao siyo waadilifu, unakuta mfuko wa saruji wa kilo 50 wanaweka kilo 49 au 47 na zile zinazopungua wanaweka kwenye mifuko mingine wanauza na hata kwenye nondo ile ya futi 40 unaweza kukuta wameweka futi 39 sasa lazima tukomeshe hali hii," alisema.

Alisema wamekubaliana na WMA kwenda kufanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye viwanda ili kuwabaini wafanyabiashara wasio waadilifu wanaopunja vipimo ili wachukuliwe hatua kali.

Alisema kuna umuhimu kwa WMA kwenda kuhakiki bidhaa hizo huko huko viwandani badala ya kusubiri ziingie sokono ndipo wakamate wafanyabiashara hao na kuwatoza faini wakati wananchi wameshaibiwa.

Mwambe alisema amefurahishwa na namna WMA inavyofanya kazi kwa weledi katika kuhudumia wateja wake, lakini alisema ni vyema ikazidi kuwa na ubunifu zaidi kila wakati.

"Wamejitahidi kusambaa nchi nzima pamoja na uchache wao na pia wamejitahidi sana kukomesha lumbesa wote mnajua lumbesa wakati ule ilikuwa maarufu sana sasa wawe wabunifu waje na mbinu mpya kila wakati," alisema.

"Sisi wizara ni walezi wa viwanda tungependa kuona viwanda vinaongezeka kwa kasi na bidhaa zinazalishwa hapa ndani kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje na kuongeza ajira kwa vijana na kuongeza wigo wa walipa kodi," aliongeza.

Alisema kuna umuhimu kwa WMA kuwa na majengo yake na kuachana na utaratibu wa kupanga hali inayosababisha kutumia fedha nyingi kulipia majengo hayo.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe (kushoto), akipokelewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Vipimo (WMA), Dk. Adelhem Meru, alipofanya ziara katika ofisi za wakala huo, jijini Dar es Salaam jana. Wa (pili kulia) ni Mjumbe wa Bodi ya wakala huo, Cosmas Ngangaji na (wa tatu kulia) ni Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Stella Kawa. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Mkurugenzi asisitiza ukusanyaji mapato

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Geofrey Mwangulumbi, amewaagiza watendaji wa kata, kusimamia ukusanyaji mapato ili kupata fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Mwangulumbi atoa agizo hilo juzi kwenye kikao cha watendaji wa kata cha kujadili vipaumbele vya mapendekezo ya bajeti ijayo (2021/22) ngazi ya kata kabla ya kuanza kwenda uongozi wa juu.

Alisema ili mapendekezo ya bajeti yafanikiwe kutekelezwa ikiwamo miradi ya maendeleo, ni lazima kuwapo na kasi ya ukusanyaji mapato na kuwaagiza watendaji wa kata wakasimamie kwa ukamilifu hilo kwenye maeneo yao.

"Tunapozungumzia masuala ya bajeti na utekelezaji wa vipaumbele vilivyoibuliwa ikiwamo miradi ya maendeleo, hapa tunazungumzia pesa, hivyo kama hakuna pesa ya kutosha utekelezaji wake utakuwa mgumu na miradi mingi haitatekelezwa.

"Hivyo nawaagiza sasa watendaji wa kata, mkaongeze kasi ya ukusanyaji mapato kwenye maeneo yenu, pamoja na kuibua vyanzo vipya, ili zipatikane fedha za kutekeleza haya tunayoyajadili ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa kila mwaka," alisema.

Mchumi wa Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga, Gwakisa Mwasyeba, aliwataka watendaji wa kata, vipaumbele vya mapendekezo yao ya bajeti ambavyo wanavitoa viguse maslahi mapana ya wananchi.

Mtendaji wa Kata ya Kitangili, Rose Matunda, akizungumza kwa niaba ya wenzake, alisema watakwenda kusimamia ukusanyaji mapato, huku akitoa wito kwa wafanyabiashara kujenga utamadunia wa kilipa mapato kwa hiari, ili serikali ipate fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo na kuwaboreshea miundombinu imara ya kufanyia biashara zao.

# DC ataka benki kuelimisha wananchi mikopo ya nyumba

**Na Hamisi Nasri, MASASI**

MKUU wa Wilaya ya Masasi, Selemani Mzee, amezitaka taasisi za fedha wilayani hapa kwenda kwa wananchi kutoa elimu ya mikopo ya ujenzi wa nyumba ili kila mwananchi mwenye kuhitaji apatiwe mkopo.

Mzee alitoa agizo hilo jana mjini hapa alipokuwa akifungua kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) kilichofanyika katika ukumbi wa zamani wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Alisema kuna uhitaji mkubwa kwa wananchi wa Masasi katika ujenzi wa nyumba za makazi, hivyo taasisi za fedha ziwe na ubunifu katika kujiendesha kwa kuwapatia mikopo wananchi ikiwamo mikopo ya ujenzi wa nyumba.

Mzee alisema iwapo taasisi hizo zitawapatia wananchi mikopo ya ujenzi wa nyumba, idadi kubwa ya wananchi watajitokeza kukopa na kuanza ujenzi kwa ajili ya kuishi na familia zao.

**Nawashauri taasisi za fedha nendeni vijijini huko mkawape elimu wananchi juu ya mikopo ya ujenzi nyumba, ili kila mwananchi awe na nyumba bora ya kuishi.**

Hata hivyo, alisema kabla ya kuanza kutoa mikopo hiyo, lazima waende vijijini ambako ndiko wananchi wengi wana uhitaji wa nyumba bora za kuishi na kutoa elimu ya mikopo.

"Nawashauri taasisi za fedha nendeni vijijini huko mkawape elimu wananchi juu ya mikopo ya ujenzi nyumba, ili kila mwananchi awe na nyumba bora ya kuishi. Kwa kweli mkianzisha huu mpango, utawainua wengi ambao wanahitaji nyumba, lakini hawana fedha taslimu," alisema.

Mzee alisema iwapo taasisi hizo, zikiwamo benki za CRDB, TPB, NBC na NMB zitaanzisha mpango huo wa kutoa mikopo ya ujenzi na kwa kwenda mbali zaidi katika mpango huo, wangeweka vifurushi vya mikopo hiyo ya ujenzi wa nyumba ili kila atakayehitaji kuingia kwenye mkopo huo aangalie kifurushi kipi kinamfaa kuendana na nyumba anayehitaji kujenga.

Alisema idadi ya wananchi kuhitaji kujenga nyumba wilayani Masasi ni kubwa, lakini kikwazo ni kuwa na fedha taslimu za kujenga, hivyo kupitia mikopo kama taasisi hizo zitaamua kuitoa, wananchi wengi watajenga nyumba na kurejesha mikopo hiyo.

Katika kutoa mikopo hiyo ikiwamo hiyo ya ujenzi wa nyumba pia kuna jambo la msingi la kuzingatia katika kutoa mikopo hiyo kwa wananchi ni suala la riba nafuu, ili kila atakayekubali kukopo arejeshe bila masikitiko ya kwa nini alikopa fedha hizo.

Mzee alisema iwapo taasisi hizo zikizingatia suala la riba wananchi wengi ambao wana uhitaji wa kukopa fedha kwa ajili ya shughuli mbalimbali kama vile biashara, kilimo na ujenzi, hawatakuwa na hofu ya kwenda kuchukua mikopo.



Sehemu ya kinamama 50 wa kiislamu kutoka Kata ya Muhungula, Halmashauri ya Mji wa Kahama, mkoani Shinyanga, wakiwa wamekalia vyerehani 10 vilivyotolewa bure na Jumuiya ya Kimataifa ya Istaqaama Muslimu Community jana, kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mkuranga kujenga stendi ya kisasa

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, imetenga zaidi ya ekari 50 kwa ajili ya kuanzisha mradi wa kimkakati wa mabasi yaendayo mikoa ya kusini na nchi za jirani.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Mhandisi Mshamu Munde, aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumzia mradi huo wa stendi ya kisasa, ambayo itajengwa Mwandege.

Munde alisema kujengwa kwa stendi hiyo, kutasaidia kuondoa kero ya stendi ya Mbagala ambayo wanaipata abiria waendao mikoa ya kusini.

"Stendi itakuwa na ukubwa wa ekari 50 na huduma mbalimbali za kijamii zitatolewa ikiwamo na maegesho ya magari," alisema.

Aliongeza kuwa baada ya kukamilika, malori, mabasi madogo na magari ya watu binafsi yatapaki katika stendi hiyo.

Munde alisema pia huduma za mabasi ya mwendokasi zitatolewa na kuongeza kuwa waliishazungumza na Wakala wa Mabasi ya Mwendokasi (DART) na wamekubaliana mabasi ya mwendokasi yatatoa huduma katika stendi hiyo.

Aliongeza kuwa stendi hiyo itakuwa na bustani ya kisasa ambapo watu wataitumia kukaa na kupiga picha na pia kutakuwa na wamachinga ambao watafanya biashara zao katika maeneo ambayo watatengewa.

"Kwa sasa mradi huo uko katika hatua za usanifu na mpaka mwishoni mwa mwezi huu, kazi za uchambuzi zitakuwa zimekamilika ikiwamo kukamilika kwa ramani," alisema.

Sambamba na hilo, alisema ramani zitapelekwa kwa taasisi za kuombea fedha, lakini si benki kutokana na kukatwaza na serikali kuomba fedha katika katika taasisi hizo.

# Hatarini kukumbwa na magonjwa ya mlipuko

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAKAZI wa Kata ya Soga wilayani Kibaha, wako kwenye hatari ya kupata magonjwa ya mlipuko kutokana na kukosa majisafi ya bomba hali inayosababisha kutumia kisima kifupi cha maji ambayo si salama.

Kutokana na hali hiyo, wananchi hao wameiomba serikali kuwakamilishia mradi wa maji unaojengwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), ili kuokoa maisha yao kwa kuwa kisima wanachotumia wakati mwingine kinakauka na kusababisha kukosa maji.

Akizungumza juzi mbele ya waandishi wa habari, mmoja wa wananchi hao, Halima Saidi, alisema kabla ya mradi huo kuanza, walikuwa wanapata maji ya DAWASA kupitia miundombinu ya zamani, lakini utekelezaji wa mradi mkubwa ulipoanza walivunja mradi wa zamani, hivyo kukosa maji.

Saidi alibainisha kuwa uhaba wa maji ulianza Novemba, mwaka jana, kipindi ambacho serikali kupitia DAWASA ilianza kutekeleza mradi wa maji kutoka Kongowe-Soga ambao mpaka sasa haujakamilika.

Naye Sophia Kassim alisema katika kata hiyo kisima kipo kimoja, hivyo kuwalazimu kuamka saa 11 alfajiri kwenda kisimani na kurejea nyumbani saa nne asubuhi kutokana na foleni ya watu.

Alisema mbali na hofu ya kupata magonjwa ya mlipuko, pia wanashindwa kufanya kazi za maendeleo kwa wakati kutokana na kutumia muda mwingi kusaka maji.

Diwani wa Soga, Shomari Juma, alisema tatizo la maji ni kubwa hasa katika vijiji vya Soga na Kipangege ambavyo walikuwa wanategemea maji ya DAWASA.

Alisema Kata ya Soga kwa sasa inakuwa kwa kasi kutokana na ongezeko la wananchi kujenga nyumba bora za kisasa zenye uhitaji wa maji mengi, lakini inakaribia miezi miwili sasa hawana maji jambo ambalo ni hatari kwa afya za wakazi wa maeneo hayo.

Juma alisema tayari amewasiliana na DAWASA ili wafanye uharaka kukamilisha mradi huo ili wananchi wapate maji. Pia aliomba kutumia njia mbadala ya kutatua kero hiyo.

Mbunge wa Kibaha Vijijini, Michael Mwakamo, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo na tayari ametembelea mradi Kongowe -Soga na kusema uko katika hatua za kukamilika.

Mwakamo alisema kwa mujibu wa wataalamu kutoka DAWASA wananchi wa Soga wataanza kupata maji Februari, mwaka huu, lakini muda huo bado mrefu.


Aliishauri DAWASA kuona namna ya kusukuma maji kupitia mtambo wa zamani kwa kuwa miundombinu yake iko vizuri ili wananchi wapate maji wakati utekelezaji wa mradi mpya ukiendelea.

Hivi karibuni, Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, akiwa katika ziara ya kukagua mtambo wa Ruvu Chini ulioko Mlandizi, alisema mradi wa Kongowe -Soga umefikia asilimia 95.

## TEHAMA jukwaa jipya demokrasia, uwajibikaji

Ukurasa 13





# siasa

JUMATANO JANUARI 13, 2021
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

Ukurasa 14

## MUSEVENI KUISHI MIAKA 40 IKULU?

# WAZIRI WA CHINA AFRIKA

## •Ni kutanguliza agenda kabla Marekani kuzinduka
## •Tanzania ya kwanza, ilianza 2013 na Rais Jinping

**Na Ani Jozeni**

WAKATI Marekani inapata taabu kungoja Rais Donald Trump, amalize muda wake Jumatano ijayo, ili kuapishwa mteule Joseph Biden, tayari China imetanguliza agenda za kuafikiana na Afrika kabla utawala mpya wa haujaingia ikulu.

Tanzania inakuwa ya kwanza kupokea ujumbe huo wa China baada ya Waziri wa Mambo ya Nje, Wang Yi, wiki iliyopita kuanzia kazi Chato alipokutana na Rais John Magufuli, ukiwa ni mwanzo wa safari ya siku tano.

Wang Yi amekaa nchini siku mbili ikionyesha kuwa, alikuwa na upana zaidi wa mazungumzo na Rais John Magufuli kuliko taifa jingine.

Kwa miaka mingi inaeleweka kuwa Tanzania ndiyo nchi ya kwanza kwa uhusiano na China, ikiendana pengine na Zimbabwe.

Hata mwaka 2013 Rais wa China Xi Jinping, alizuru Tanzania likiwa ni taifa la kwanza tangu alipoapishwa kuwa kiongozi wa nchi hiyo.

Rais John Magufuli, akizungumza kwenye mkutano na Waziri wa Mambo ya Nje wa China Wang Yi, aliomba China iisamehe Tanzania madeni ya dola takriban dola milioni 167.7zilizokopwa kujenga reli ya TAZARA, kiwanda cha nguo cha Urafiki na nyumba za wanajeshi.

Ni suala ambalo China haikulitolea maelezo, lakini Waziri Yi, alilipokea.

Aidha, China imekubali kusaidia ukamilishaji wa ujenzi wa reli ya kisasa SGR ulioafikiwa kwa kujenga kipande kinachoanzia Mwanza hadi Isaka mkoani Shinyanga chenye urefu wa kilomita 341.

Baada ya Tanzania Waziri Yi aliendelea na safari kuelekea Seashells, Nigeria, Botswana na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.



Rais John Magufuli, akimsikiliza Mjumbe wa Baraza la Taifa na Waziri wa Mambo ya Nje ya China, Wang Yi, baada ya kufanya mazungumzo na kushuhudia utiwaji saini wa mkataba wa ujenzi wa reli ya Mwanza-Isaka katika Ikulu ndogo ya Chato mkoani Geita Januari 8, 2021. **PICHA: IKULU**

### AJENDA YA CHINA

Itachukua miezi kadhaa kwa serikali mpya Washington kujipanga na kuanzisha sera zinazoeleweka, ingawa sasa kuna picha kuwa Biden atakuwa na nguvu zaidi kuliko ilivyotazamiwa hapo awali.

Ni baada ya Chama cha Democratic cha Biden kushinda uchaguzi wa viti vya Senate Jimbo la Georgia ambako wakati wa uchaguzi mkuu wa Novemba hakuna aliyefikia asilimia 50, kati yake na Donald Trump.

Yako maeneo ambayo China inaweza kuhitaji kufahamu, kwa mfano kuanza kutumika kwa Mkataba wa Soko Huria Afrika (CAFTA) ambao umeanza rasmi kutumika Januari mosi baada ya nchi 33 kuupitisha bungeni.

Tanzania ilitia saini, lakini bado ulikuwa haujaingia katika sheria, ila unaweza kuwa wa manufaa kwa China katika uendelezaji wa ule mkakati wa 'belt and road,' (ukanda na barabara) yaani kwa uwekezaji na uuzaji wa bidhaa zake.

Kwa upande wa China mkwamo wa kisiasa Marekani kuna faidi kwani sura ya Marekani nchi za nje imekuwa na mkanganyiko wa Rais Trump kuwahamisha wafuasi wake kushambulia bunge na kuua polisi.

Rais mteule wa Marekani alisema katika hotuba kuhusu tukio hilo kuwa ingekuwa ni maandamano ya 'Black Lives Matter,' yamefikia hatua ya kuvuruga kinachoendelea bungeni, kujaribu kuzuia kumthibitisha rais mteule kuwa ameshinda uchaguzi mkuu, 'wangepata taabu sana.'

Lakini kwa vile ilikuwa ni kundi kubwa la weupe (Wazungu) wanaoapa kwa jina la Trump polisi hawakufanya linalotakiwa, walikuwa wachache na mmoja akapoteza maisha.

Ni jambo ambalo limevuruga sura ya Marekani mbele ya dunia na itachukua muda kiasi kwa serikali mpya kuingia madarakani na kila kitu kionekane kinaenda sawa dunia ianze kuisikiliza Marekani.

Ni kawaida katika uhusiano wa nchi za nje kuwa kiwango cha umoja ndani ya nchi kina athari kubwa katika uwezo wa kuendesha siasa au uhusiano na nchi za nje.

Pale ambako kuna mianya ya wazi katika utii kwa utawala uliopo madarakani, nchi kama hiyo haiwezi kuendesha uhusiano wa nje kwa urahisi, kwani nchi nyingine (serikali zao) hazitaamini au kutilia maanani serikali hiyo iliyoko mashakani inachoongea.

Kwa mfano Ijumaa iliyopita, asubuhi kwa saa za Marekani, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Nancy Pelosi, aliongeza na mkuu wa majeshi wa Marekani, kuhofia Trump,' akatoa amri ya kushambulia mahali fulani, hata kutumia bomu la nuklia.

Taarifa zilisema Spika hakujibiwa.

### ZIARA YA WANG YI

Ziara ya Waziri wa Mambo ya Nje wa China haikufuatana na mkasa huo jijini Washington, lakini ni wazi ungechangia hoja za Wang Yi kwa nchi za Afrika kuwa China ni nchi thabiti yenye sera zinazoeleweka inayoweza kufanya mikataba ya muda mrefu na Afrika kuliko taifa jingine.

Marekani, kwa upande wa pili, hivi sasa imegubikwa na sintofahamu ya kuwa na pande mbili za kisiasa zinazohasimiana, na hivyo kujiweka njia panda ikingoja lini utawala uliopo madarakani utaisha, uingie mwingine, tofauti na uliotangulia.

Wakati Rais Barack Obama alitaka 'mabadiliko,' Trump aliingia kama kinyume cha Obama na sasa Biden kama kinyume cha Trump.

Pia kuna uhusiano kwa kiasi fulani kati ya mahitaji ya China kwa nchi za Afrika hivi sasa na historia ya uhusiano ya pande hizi mbili, kuwa Afrika ilikuwa ndiyo kundi kubwa zaidi Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kutaka China ichukue nafasi ya Taiwan, kisiwa kinachojitawala, lakini kwa jadi ni sehemu ya China.

### KUIPINGA CHINA

Utawala wa Trump umejitahidi kuitenga China katika maeneo tofauti ya kibiashara na hasa matumizi ya teknolojia au vifaa vya kisasa vya mawasiliano kutoka China (5G) vya kampuni ya Huawei, ukisema kampuni hiyo ina uhusiano wa karibu na Jeshi la China na inaweza kuitumia kijasusi.

Ni eneo ambalo Trump alishindwa kuwaridhisha kihoja hata washirika wake wa karibu zaidi, nchi za Ulaya.

Maeneo ya ushindani kati ya Marekani na China kibiashara barani Afrika yanapungua au labda hayapo kwani ni kampuni chache za Marekani zinafanya biashara kubwa na hata kwingineko Afrika siyo kampuni nyingi.

Ila Marekani ni kitovu cha biashara ya fedha duniani na kila nchi, hata China inategemea soko la hisa na fedha la Marekani iinue mikopo kutumia katika ustawishaji wa viwanda au teknolojia.

Inatazamiwa kuwa kampuni za China zilizoondolewa katika soko la mitaji New York zinaweza kurudishwa kama sehemu ya kupangua sera za Trump.

# Mbunge anapotangaza kujichimbia jimboni

## •Aahidi hatawaacha 'yatima' wapigakura



Mbunge wa Butiama (mwenye miwani), akikabidhi moja ya magunia yenye vipande vya miti ya mihongo aina ya mkombozi, kwa ajili ya kuboresha kilimo cha zao hilo jimboni mwake.

**Na Sabato Kasika**

HOFU ya wananchi na kilio cha kukimbiwa na wabunge waliowachagua kwa awamu kadhaa imemlazimisha Mbunge Jumanne Sagini, kupinga kambi jimboni Butiama kuwahudumia wapigakura wake.

Anaiambia Nipashe kuwa hatua hiyo inalenga kuwaondolea hofu wananchi, ambao walidhani huenda baada ya kumchagua angeingia mitini.

"Wakati wa kuomba kura niliahidi kuwa karibu tena kushirikiana nao kutatua kero zao na kuwaletea maendeleo na hilo nimeanza kulitimiza kwa kuwatembelea kila kata," anasema Sagini.

Katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, Sagini ni miongoni mwa wana CCM, waliopita bila kupingwa na kuwa mbunge wa Butiama, akitanguliwa na Nimrod Mkono, aliyeongoza jimbo hilo kwa miaka 20 ambalo awali lilikuwa Musoma Vijijini, lakini 2015 liligawanywa na kupatikana jingine la Butiama.

Anasema baada ya kiapo amepiga kambi jimboni mwake, ili kusikiliza kero za wananchi na kushirikiana nao kuzitatua ikiwa ni moja ya ahadi zake alizoahidi wakati wa kampeni na anatarajia kuzuru kata zote zikiwamo Bisumwa, Buhemba, Bukabwa, Buruma na Busegwe.

"Nimefanya ziara katika jimbo langu ili pia kuhamasisha jamii katika shughuli za maendeleo, kwani ushirikishwaji ni muhimu, mbunge kukaa mbali na wananchi wangu kwa muda mrefu si jambo jema," anasema.

### KERO ALIZOTATUA

Anasema: "Butiama kama yalivyo majimbo mengine, inakabiliwa na matatizo mbalimbali ambayo yanahitaji utatuzi mfano kilimo cha mihogo kinakabiliwa na ugonjwa unaosababisha wakulima wasipate tija," anasema mbunge huyo.

Anasema, hali hiyo imemfanya anunue magunia 80 ya mbegu ya mihogo aina ya mkombozi yenye thamani ya zaidi ya Sh. 2,000,000 na kuwagawia wakulima na kwamba Butiama inategemea mihogo, viazi vitamu na viazi lishe, mahindi, mpunga na mtama, lakini matatizo yanabakia kwenye mihogo.

"Wataalamu wa kilimo wanasema, mbegu ya mkombozi inahimili magonjwa na inaweza kutoa magunia kati ya 16 hadi 20 katika ekari moja, tofauti na nyingine zinazotoa magunia matano hadi sita kwa ekari," anasema mbunge huyo.

Aidha, anafafanua kuwa michezo kwa sasa ni ajira, na kwamba ameshagawa mipira 40 kwa timu mbalimbali katika kata 18 za jimbo hilo ikiwa ni maandalizi ya mashindano ya mpira wa miguu ili kuinua vipaji vya soka.

"Nitaendelea kuibua michezo mbalimbali jimboni, kwa kuwa michezo kwa sasa ni ajira, na nitatafuta baiskeli 20 kwa rafiki zangu ili kuanzisha mashindano ambayo ni sehemu ya ajira," anasema.

Anataja ujenzi wa shule ambao ameshirikiana na wananchi akitoa mifuko 255 za saruji kwenye kata za Kamugegi na Nyamimange ili kuboresha miundombinu ya shule kata hizo.

### VIPI MAJI JIMBONI?

Anasema, Wizara ya Maji imesaini mkataba wa kujenga mradi mkubwa wa maji kutoka Mugango Musoma Vijijini hadi Kiabakari jimboni humo unaotarajia kukamilika baada ya miezi 24 na kuanza kuhudumia wananchi 200,000 kwenye vijiji 19 vilivyopo wilaya za Musoma na Butiama.

"Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Antony Sanga, ameshasema kuwa mradi huo ukikamilika utatoa huduma ya maji kwa wananchi kwa miaka 20 kwa utoshelevu, na utazalisha lita zaidi ya milioni 17 kwa siku katika awamu ya kwanza," anasema mbunge huyo.

Anamkariri Katibu Mkuu kuwa mahitaji ni lita milioni 12 kwa siku, na kwamba kwa awamu ya pili uzalishaji utakuwa lita zaidi ya milioni 35, huku baadhi ya vijiji vikiongezwa kwenye mradi huo.

"Baadhi ya vijiji vya jimbo langu vitanufaika na mradi huo, wakazi wa Butiama wataondokana na adha ya maji inayowakabili kwa sasa baada ya mradi huo kukamilika," anasema.


Anafafanua kuwa ilikuwa ni aibu kuona maji yanakwenda mbali zaidi ya kilometa 400 mikoa ya mbali, huku wananchi wa Butiama na Musoma wanakosa huduna hiyo wakati wanazungukwa na Ziwa Victoria.

"Nimshukuru Rais Dk. John Magufuli kwa uamuzi wake wa kuleta mradi huu haraka iwezekanavyo baada ya kuapishwa, hakika amejibu ombi na kilio cha wananchi, niombe pia kata zinazopakana na mto Mara ikiwamo kata ya Buswahili na Bukabwa ikiwezekana ziangaliwe nazo ziwekwe kwenye mradi awamu nyingine, wananchi wapelekewe huduma ya maji," anasema.

### HISTORIA YA BUTIAMA

Sagini anatamani kuiona Butiama mpya akieleza kuwa ni sehemu muhimu kwa taifa kwani ndiko kilipo Kijiji cha Mwitongo alipozaliwa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1922 na ni wilaya ilioanzishwa rasmi Machi 2012 ikiwa ni sehemu ya kuvutia utalii hasa wanaozuru Makumbusho ya Mwalimu Nyerere pamoja na kujifunza historia yake.

Anakusudia kushirikiana na wapigakura wake ili kuifanya iwe ya kisasa na yenye maendeleo makubwa. Sensa ya mwaka wa 2012, inataja idadi ya wakazi kuwa ni 241,732 wanaojishughulisha na kilimo cha mazao ya chakula na biashara.



Mbunge wa Butiama (katikati), akiwa katika moja ya mikutano yake jimboni.

# TEHAMA jukwaa jipya demokrasia, uwajibikaji

**Na Mwandishi Wetu**

TEKNOLOJIA ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inatajwa kuwa ni moja ya nyenzo zinazoweza kuongeza uwajibikaji na demokrasia barani Afrika wakati uhusiano baina ya serikali na wadau wa kiraia unapokuwa na ukakasi.

TEHAMA inakuwa mbadala pale serikali zinabana uhuru wa asasi za kiraia, vyombo vya habari na kutumia sheria kandamiza kudhibiti uhuru wa maoni, kuhoji na kukosoa mienendo ya dola.

Hayo ni baadhi ya masuala yanayoelezwa Asasi za Kiraia (azaki) za Afrika Mashariki kwenye mkutano wa kujadili namna ya kufikisha ajenda zao kwenye maendeleo ya mataifa yao, kupitia uwanja wa vyama vya kiraia.

Wafula Nafula kutoka Baraza la Vijana la Jumuiya ya Madola (Common Wealth Youth Council), anasema TEHAMA ni njia bora ya kuzibana serikali kusikiliza raia, kuongeza uwajibikaji, kuheshimu haki za binadamu na kuwa karibu na wananchi.

Anatoa mfano wa vuguvugu la kutaka kulinda maisha ya Waamerika Weusi la 'Black Lives Matter' kuwa limekuwa mtandao wa kimataifa, unaounganisha sehemu kubwa ya dunia kudai haki na ulinzi wa raia bila kujali kaliba wala rangi.

Wafula kutoka Kenya anasema TEHAMA ni uwanja mpya wa kudumisha uhuru wa maoni, kudai haki, kupinga ukandamizi, kupiga vita uongozi wa mabavu na kila aina ya dhuluma.

"Kupitia mitandao ya kijamii wananchi wanaongea bila kubanwa, kutumia picha na sauti za video, hotuba, kuuliza maswali na kupeana taarifa muhimu ambazo awali wasingezipata kutoka na kudaiwa kuwa ni za siri," anasema Wafula.

TEHAMA ndiyo mitandao ya kijamii ndilo jukwaa jingine la raia kufanyakazi za maendeleo ambazo serikali imeshindwa au imekwama, akitoa mfano:

"Watu wanachanga fedha kufanikisha matibabu ya wagonjwa, nje na ndani ya nchi. Wanasaidia waathirika wa majanga. Wanawapatia huduma mbalimbali kuanzia vyakula na dawa. Yote hayo ni mshikamano wa kiraia ambao ni fursa zinazoweza kutumiwa na asasi za kiraia uwanja unapobanwa."

Akitoa mchango wake Richard Ssewakiryanga Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mafunzo ya MS TCDC ya Arusha, anayezungumzia uzoefu wa azaki za Uganda, anasema ni jukumu la vyama hivyo kushauri serikali, kusimamia matumizi ya rasilimali za taifa kwa umakini, kuongeza uwajibikaji na kufuatilia mienendo ya uongozi wa umma.

"Zinawajibika kuhoji matumizi ya fedha za umma mathalan, Afrika ina wanasiasa ambao wakiwa kwa wapigakura ni kama malaika wanahimiza na kuchangia maendeleo na kusaidia wananchi kutatua matatizo. Hata hivyo, wakiwa ndani ya ofisi za umma ni wabadhirifu, bungeni wanapitisha mikataba tata na kutunga sheria kandamizi zinazoumiza raia."

Anasema na kuongeza:

"Hii ni ajabu ni kuwaibia wapigakura ambao wakiwa nao jimboni wanawapenda na kuwasikiliza, lakini wakiondoka wanawahujumu na kuwaongezea umaskini." Anakumbusha kuwa wajibu wa azaki katika hilo ni kuibua tuhuma zao na kudai uwajibikaji na utumishi wenye maadili kwa vile mganga hajigangi, serikali zinahitaji jicho la pembeni kuzisimamia na hiyo ndiyo demokrasia.

Anasema kila wakati serikali zinakuwa na hofu dhidi ya azaki kutokana na kufikiri kuwa zinakosolewa na huenda zikakataliwa na wananchi, lakini sivyo, nia ni kuongeza uwajibikaji na kuleta maendeleo na kwa vile serikali zenyewe haziwezi kufanya kila jambo ni lazima zipate washirika ambazo ni taasisi za kiraia.

Washiriki wa jukwaa la azaki wakiwamo kutoka Kenya, Uganda, Tanzania na Rwanda, wanagusia kuwa mwaka 2020 ulikuwa wa uchaguzi kwa nchi nyingi za Afrika kama Tanzania, Burundi na sasa ni zamu ya Uganda, lakini muda wa uchaguzi dola linadaiwa kuweka mazingira yanayopunguza kukosolewa na wakati mwingine kubana wadau wanaofuatilia zikiwamo azaki na wakati mwingine kuzifuta au hata kuziwekea sheria na mazingira magumu, zikichukuliwa kama maadui wa taifa.

> "Watu wanachanga fedha kufanikisha matibabu ya wagonjwa, nje na ndani ya nchi. Wanasaidia waathirika wa majanga. Wanawapatia huduma mbalimbali kuanzia vyakula na dawa. Yote hayo ni mshikamano wa kiraia ambao ni fursa zinazoweza kutumiwa na asasi za kiraia uwanja unapobanwa."

Lakini, taasisi hizo za kiraia zinazikumbusha serikali kuacha malumbano baina yao kwa vile azaki zinatimiza jukumu la kusaidia kuhudumia raia kwa kushirikiana na vyombo vingine kufikisha huduma muhimu ambazo dola peke yake lisingeweza.

Wakijadili nafasi ya mashiriki ya kiraia katika nchi zao wanasema kumekuwa na msuguano kati ya serikali na wadau hao jambo linalofanya uwanja na nafasi za kiraia kusinyaa licha ya kwamba katiba zinaruhusu na kutoa haki kwa raia kufanya majukumu yao.

Mathalani sura ya kwanza, ya Katiba ya Tanzania ibara ya 12 hadi 24 zinaelezea haki za muhimu za binadamu na ibara ya 25 hadi 28 inazungumzia wajibu wa muhimu kwa raia ambazo zinahusiana na tamko la haki za binadamu vyote hivyo wanaeleza kuwa vinaonyesha kuwa taifa linaheshimu haki za binadamu na kuenzi kuwapo demokrasia na ustawi wa raia.

Kwa mfano, raia wana haki na uhuru wa kukusanyika, kuwa wanachama wa vyama wanavyovipenda, kutoa na kupokea maoni, kuabudu na kufanyakazi hivyo kwa mujibu wa sura ya tatu ya katiba ya vyama vya kiraia ni haki ya wananchi, hivyo uwapo wake ni muhimu kusaidia serikali kwenye maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa huduma pale wanapoona zinahitajika, kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu kampeni za haki za binadamu na kupinga ukatili ukiwa kijinsia, kuondoa uonevu kwa watoto kama kuhamasisha kuepuka mimba na ndoa za utotoni, kupinga mila na utamaduni wa kudhalilisha na kukandamiza wanawake na mabinti.

Kwa hiyo azaki zinataka uwanja mpana ili zisaidie kufikisha elimu kwa wanaoikosa, kuwapa chakula, makazi na vifaa muhimu, kuhudumia wahitaji, kutoa tiba, kuhudumiwa wanaotumia dawa za kulevya kuachana na mihadarati kwa kuwatunza ndani ya nyumba za mabadiliko (sober houses), kuwaondoa watoto kwenye kazi hatarishi mfano 'nyoka' wanaotumiwa kuchimba madini migodi, kukemea ajira mbaya za watoto, kuwanyanyasa kingono hasa kwenye madanguro na nyumba za kuonyeshea picha za video mitaani.

Kwa mtizamo huo azaki zinataja kuwa zina umuhimu na mchango mkubwa kwa jamii na ni wakati wa serikali kuthamini umuhimu wake badala ya kuzichukulia kama maadui wa taifa na au mawakala wa mataifa ya kigeni wanaofanyakazi kwa niaba ya serikali zao.

Israeli Ilunde, Youth Partnership Countrywide, anazikumbusha azaki kushirikiana na serikali na kutimiza wajibu kwa misingi ya kisheria kwa mfano kuwasilisha taarifa za mkutano mkuu wa mwaka, ripoti za fedha, kutii na kuieleza serikali kile wanachofanya na mafanikio wanayopata.

Uhuru wa kiraia wa kila mwananchi kuwa na maoni yake, kujumuika na wengine na kuwa mwanachama wa asasi, au jumuiya yoyote anayoipenda ndiko kunakoupa mashirika yasiyo ya kiserikali kufanyakazi kwa mujibu wa katiba ni suala ambalo limekuwa likishindaniwa baina ya serikali (dola) na asasi za kiraia na kwamba hakuna taifa ambalo litawaachilia wadau kufanya wapendavyo.

Lakini wadau hao wanaona kuwa wakati umefika kwa serikali kufahamu kuwa kila raia ana haki kwa mujibu wa katiba na mikataba ya kimataifa na kwamba kushirikiana kufikia azma hiyo ndilo jukumu la kila mmoja kwa vile wote wanategemeana.

Kepta Ombeti kutoka Kenya anakumbusha kuwa ili kuwa na demokrasia serikali na dola vinahitaji kusikia sauti za wananchi ambazo hupazwa kupitia asasi za kiraia zikizungumzia upatikanaji wa dawa hospitalini, elimu bora, maji safi na salama, barabara na haki zote za msingi.

Mengine ni masuala ya sheria kandamizi, uharibifu wa mazingira na serikali kuficha taarifa muhimu ambazo zinahitajika kwa wananchi, kudai katiba mpya, tume huru za uchaguzi, uhuru wa kisiasa na kuheshimu maoni na haki za raia na kwamba kuwa na uwanja wa kumulika serikali kupata majibu iwapo malengo yake yanafanana na kile kinachofanywa na vyombo vya dola, haukwepeki.



Wadau wa AZAKI za Afrika Mashariki kwenye jukwaa la kutathimini mchango wa taasisi za kiraia lililofanyika Arusha. **PICHA: MWANDISHI WETU.**

## JUKWAA LA UONGOZI



Mahasimu Yoweri Museveni (kulia) na Bobi Wine, wanachuana leo kwenye uchaguzi mkuu wa Uganda. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# MUSEVENI KUISHI MIAKA 40 IKULU?

## •Bobi Wine 'rais wa ghetto' kumbabua?

**Na Mwandishi Wetu**

LEO ndio leo siku ambayo maswali hayo yatakapojibiwa. Wapigakura wataamua iwapo Rais Yoweri Museveni, ambaye ni miongoni mwa marais wa Afrika waliongoza muda mrefu atafanikiwa kuitawala Uganda kwa miaka 40.

Akiwa amechukua nchi mwaka 1986 kutoka Chama cha National Resistance Movement (NRM), ameliongoza taifa hilo kwa miaka 35 na endapo atafanikiwa kushinda uchaguzi wa leo na kukaa ikulu kwa miaka mingine mitano ataandika historia ya kuwa rais wa nchi aliyeongoza kwa nusu karne.

Mpinzani wake mkuu ni Bobi Wine au Robert Kyagulanyi Ssentamu, ambaye kwa mara ya kwanza amekuwa tishio kwa kiongozi huyo, anayeamini kuwa ndiye pekee anayeweza kuliongoza taifa hilo la Afrika Mashariki, anamtikisa akijiita 'rais wa ghetto'.

Anajiamini kwa sababu anaungwa mkono na vijana wengi aliowahamasisha kuwa wanahitaji mabadiliko na kuwa na kiongozi anayetoka kwenye umaskini ili kuwakomboa.

UCHAGUZI KUWA HURU?

Ni swali linalojibiwa na Makala ya DW, likisema kuwa Waganda wana mashaka kama uchaguzi huo utakuwa wa huru na haki.

Licha ya kwamba joto la uchaguzi nchini Uganda ni kali kila mahala kutokana na matamshi ya wanasiasa pamoja na askari wa jeshi na polisi wanaonekana kila mahala wakiwa wamejihami kama ambao wanaelekea vitani, hakuna Imani kuwa utakuwa huru.

Wananchi wenyewe wanaonekana kujiandaa kwa hali ambayo wengi wanahisi uchaguzi utakuwa wa ushindani mkali nap engine wenye vurugu na machafuko.

Sheikh Abdallah Sabiila Kadhi wa Sebei, ananukuliwa akisema vyombo vya dola vimetumiwa kupindukia kukandamiza wapinzani na upinzani umejaribu kukabiliana nao kulinda maslahi yao.

Anasema kwa hali hiyo patakuwa na mapambano kwa sababu kuna msemo kuwa mgombea wa NRM lazima ashinde kwa vyovyote vile.

DW inaeleza kuwa upinzani unalaumu utawala wa Rais Museveni kwa kuleta sintofahamu na kusababisha hofu nchini Uganda.

Viongozi wa upinzani wana mtazamo kuwa utawala wa Rais Museveni ndiyo ulaumiwe kwa hali hii ya taharuki iliyotanda na kuwasababisha wananchi kuingiwa na hofu.

"Uchaguzi usichukuliwe kuwa vita ili tutazamane kama watu walio katika uwanja wa mapigano kwani majeshi yamedhibiti kila suala la uchaguzi huo na kwa hiyo hauwezi kuwa huru wala haki," anasema Winnie Kiiza Mratibu wa Kampeni wa Chama cha ANT

Wanaharakati wa haki za binadamu kwa upande wao tangu wiki iliyopita walianza kueleza kuhofia usalama wao nchini Uganda.

Wanasema kinachoshangaza ni kwamba hata Rais Museveni mwenyewe anashuku kwamba kuna njama za udanganyifu kufanyika ili kumsababisha asishinde katika uchaguzi huu.

Museveni anasema kuna watu wanaopanga kuiba kura wakiwamo maofisa wa uchaguzi ambao watapewa rushwa kubadili matokeo.

Lakini baadhi ya wapinzani, wanamtaka Rais Museveni akubali matokeo ya uchaguzi endapo atashindwa na aonyeshe uzalendo kwa kukabidhi madaraka kwa amani.

La sivyo, itamaanisha kuwa yeye hajali kama nchi itatumbukia katika hali ya sintofahamu wakimkumbusha kuwa mwaka 1980, Museveni ndiye aliitumbukiza Uganda katika sintofahamu iliyodumu miaka mitano na kusababisha vifo vya mamia ya watu pale alipopinga matokeo ya uchaguzi na kuanzisha harakati za kumwondoa Rais aliyetangazwa mshindi, Milton Obote.

### KANUNI MPYA ZAHOJIWA

Wakati huo huo, upinzani na baadhi ya wagombea kwa upande wa utawala aidha wameikosoa Tume ya Uchaguzi kwa kanuni mpya ambazo imezitoa hivi karibuni.

Tume hiyo imetishia kufutilia mbali matokeo ya uchaguzi ya kituo chochote ambacho watu watakataa kuondoka baada ya kupiga kura na pia hakuna mtu atakubaliwa kwenda na simu kwenye vituo hivyo.

Wadau wanaelezea kuwa simu zitasaidia katika kuwasilisha na hata kuhifadhi ushahidi wa vitendo vyovyote vitavyoweza kuathiri matokeo ya uchaguzi.

### VUGUVUGU LA BOBI WINE

Bobi Wine au Robert Kyagulanyi Ssentamu, mwaka 2008, aliachilia kibao maarufu kama 'Kiwani' na hakuna aliyekuwa na mawazo kwamba mbunge huyu wa Jimbo la Kyadondo Mashariki, angekuja kuwa mwanasiasa mashuhuri na kumkalia kooni Rais Yoweri Museveni.

Mwanamuziki huyo amekuwa mshindani namba moja wa Rais Yoweri Museveni na chama chake cha NRM katika uchaguzi mkuu wa Uganda ambao leo unaamua hatima ya mahasimu hao.

Miaka kadhaa iliyopita, Bobi Wine alikuwa akijulikana kwa kuimba nyimbo zinazoeleza maisha ya watu maskini yeye mwenyewe akiwa amezaliwa na kukulia katika mazingira ya kimaskini huko Kamwokya.

Hilo ndilo jambo lililompa umaarufu mkubwa miongoni mwa wananchi wa taifa hilo ambao wengi wao ni masikini.

Ni dhahiri kuwa wengi wamepigwa na butwaa walipoanza kusikia habari za Bobi Wine kuwa ni mwana siasa aliyepamba moto na kushangaa zaidi waliposikia amefanikiwa kuwa mbunge mwaka 2017; akiwa mgombea binafsi huku akiwabwaga wagombea wa vyama vikuu vya NRM cha Museveni na FDC vilivyokuwa na wagombea maarufu kwenye jimbo hilo.

### UMAARUFU

Nini hasa kimemfanya mwanamuziki huyu mashuhuri aliyekuwa akisifika kwa kuimba nyimbo za kimapinduzi na kujiita ''Rais wa ghetto' kubadilika na kuwa mshindani wa kipekee dhidi ya utawala wa takribani miongo minne wa NRM.

Pengine ni kuwatetea na kuwazungumzia maskini ambao ni vijana.

Bobi Wine ni miongoni mwa wagombea 10 wanaochuana na Museveni.

Akiwa na miaka 38 na kujibandika jina la "rais wa ghetto", ni mwana muziki maarufu Afrika Mashariki ambaye ameng'ara vikali na amefanikiwa kisiasa baada ya kuwahamasisha vijana na wengi kumkubali na kumuunga mkono na kutaka awe rais wao.

Bobi Wine amekuwa mkali na mkosoaji mkali wa Museveni akimwambia kuwa anawaogopa wananchi na kwamba yeye hamhofii.

*DW/BBC*



## HABARI DODOMA

# Halmashauri yabaini shida machinga stendi ya mabasi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imemwagiza Meneja wa Kituo Kikuu cha Mabasi Dodoma, kuweka utaratibu mzuri kwa ajili ya wajasiriamali kufanya shughuli zao kituoni huko.

Agizo hilo lilitolewa jana na Meya wa Jiji hilo, Profesa Davis Mwamfupe, alipotembelea kituo hicho kwa lengo la kujionea hali ya huduma.

Profesa Mwamfupe alisema amebaini kuwapo mrundikano wa bidhaa katika eneo la kituo hicho, jambo ambalo linapaswa kuwekewa utaratibu.

Alimtaka meneja wa kituo hicho kuweka utaratibu mzuri kwa ajili wajasiriamali kutokana na kufanya biashara kwenye kumbi za abiria.

"Kuna mrundikano wa bidhaa za wajasiriamali katika maeneo mbalimbali kituoni hapa, hasa katika kumbi za kukaa na kusubiria mabasi abiria na bidhaa zilizoenea katika njia zilizotengwa kwa ajili ya abiria kupita ni tatizo," alisema.

Mmoja wa abiria waliozungumza na Nipashe kituoni huko, Juliana Nyoni, alisema utaratibu mzuri unatakiwa kuandaliwa ili abiria wasipate bugudha na kulinda usalama wa mali zao.

"Utaratibu huo uende sambamba na wafanyabiashara wadogo kufanya biashara zao katika maeneo waliyotengewa ili kutosababisha adha kwa watumiaji wengine wa kituo cha mabasi," alishauri.

# TANESCO yataja kiini umeme kukatika

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Umeme (TANESCO) Mkoa wa Dodoma, limesema kukatika kwa umeme mara kwa mara kwenye baadhi ya maeneo kumetokana na wananchi kuchoma nguzo za umeme wakati wa kiangazi.

Kutokana na kikwazo hicho, shirika hilo limewataka wananchi kuhakikisha wanapochoma nyasi, wazingatie umbali wa hatua 10 kutoka kwenye nguzo.

Meneja wa TANESCO mkoani hapa, Frank Chambua, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema baadhi ya wananchi wakati wa kiangazi wamekuwa wakichoma nyasi karibu na nguzo za umeme, jambo linalochangia nguzo nyingi kupata hitilafu na kuliwa na mchwa.

**Kituo cha NARCO Kongwa kikikamilika na kuanza kufanya kazi, kitasaidia kupunguza tatizo la kukatika umeme mara kwa mara katika njia hiyo.**

"Unakuta nguzo zaidi ya 40 kwa siku zimedondoka chini katika maeneo mbalimbali, suala hilo linachangia tatizo la umeme kukatika katika eneo, husika kwa sababu tayari kunakuwa na uharibifu wa miundombinu hiyo," alisema.

Alisema TANESCO itaendelea kutoa elimu kwa wananchi katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha wanajua umuhimu wa kutoharibu miundombinu hiyo, ili wasisababishe hitilafu za umeme.

Aliwataka wananchi walio pembezoni kuhakikisha kila mmoja anakuwa mlinzi wa mwenzake ikiwamo kutoa taarifa pale wanapoona kuna uharibifu wa miundombinu inayojengwa na shirika kwa ajili ya kusambaza umeme.

Akizungumzia shida ya njia ya Mpwapwa kukatika umeme mara kwa mara, meneja huyo alisema inatumia kituo cha kupoza umeme cha Zuzu, hivyo kila kunapohitajika kufanya matengenezo, lazima umeme ukatwe kwa muda.

"Kituo cha NARCO Kongwa kikikamilika na kuanza kufanya kazi, kitasaidia kupunguza tatizo la kukatika umeme mara kwa mara katika njia hiyo," alisema Chambua.

"Mpwapwa kuna njia moja inatoka Kilolo mkoani Iringa na inatoa huduma baadhi ya maeneo pamoja na kituo kingine kidogo cha kusambaza umeme kinajengwa Mtera, vyote vipo katika hatua za mwisho, vitasambaza umeme katika Wilaya ya Mpwapwa," aliongeza.



Msukuma toroli akipita kwa shida kwenye soko la Sabasaba, jijini Dodoma jana, kutokana na kujaa maji machafu na tope, lililosababishwa na mvua kubwa inayoendelea kunyesha katika Jiji hilo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# 'Vijana changamkieni mikopo ya halmashauri'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Endless Success, amewataka vijana kutumia fursa ya mikopo inayotolewa na halmashauri nchini, ili kujikwamua kiuchumi badala ya kukaa vijiweni na kujiingiza kwenye uhalifu.

Amina Feruz alitoa rai hiyo jana, wakati wa warsha iliyoandaliwa na taasisi hiyo jijini hapa, akisema halmashauri zinatoa fedha hizo ili kuwasaidia vijana kupanua wigo wa kuendeleza shughuli za ujasiriamali badala ya kutegemea ajira pekee.

Aliwataka vijana kuunda vikundi kuchangamkia fursa hiyo ambayo itawasaidia kuwapa mwongozo wa kubadili fikra potofu ya kusubiri kuajiriwa.

"Vijana tumieni fursa ya mikopo inayotolewa na serikali kupitia halmashauri, kubuni miradi ya kufanya, hii itawasaidia kujikwamua kiuchumi badala ya kusubiri ajira.

"Awali, sheria ya utoaji mikopo ya asilimia 10 katika halmashauri wakopaji walilazimika kuwa na biashara, lakini hivi sasa sheria hiyo inaelekeza mtu kuwa na andiko la mradi anaotaka kufanya kupitia mkopo anaotarajia kukopa, lakini awapo kwenye kikundi," alisema.

Alisema taasisi yao ipo kwa ajili ya kuwapa mwongozo vikundi vya vijana ya namna ya kupata mikopo hiyo ikiwamo kuwakutanisha na wataalamu kulingana na mradi wanaohitaji kufanya.

Mkurugenzi huyo alisema taasisi yao pia hufanya kazi ya kutoa elimu ya usimamizi wa fedha kwa vikundi vya vijana ambao wako katika taratibu za uchukuaji mikopo ya kufanyia biashara zao.

Mmoja wa washiriki wa warsha hiyo, Juma Mrisho, aliishukuru halmashauri kwa kubadili sheria ya utoaji mikopo kwa vijana, akisema itachangia vijana kubuni miradi ya biashara yenye matokeo chanya.

Mrisho alisema vijana wengi wana uwezo wa kufanya biashara katika maeneo wanayotoka, lakini tatizo kubwa linalowakabili ni ukosefu wa mitaji.

Mikopo ya serikali imewarahisishia badala ya kuwa na biashara zisizo na mwongozo mzuri, sasa wanawasilisha wazo lenye michanganuo iliyojadiliwa na kupitishwa.

"Mabadiliko ya sheria hii yatawasaidia sana vijana kuendesha ujasiriamali badala ya kukaa vijiweni," alisema Mrisho.

Alisema hakuna sababu ya vijana kulalamika ugumu wa maisha na ukosefu wa ajira, akisisitiza kuwa kinachotakiwa ni kubuni wazo lenye tija ambalo litawasaidia kupata mkopo na kuendesha biashara walizokusudia kufanya.





# RC akomaa wafugaji kutoa mifugo kwenye ranchi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amesisitiza kusimamia agizo lake la kuwapa siku sita wafugaji kuondosha mifugo kwenye ranchi za Usangu, mashamba ya Ihefu na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Chalamila alitoa agizo la kuwataka wafugaji kuondoka katika ranchi hiyo mwishoni mwa wiki akiwa wilayani Mbarali mkoani Mbeya.

Hivyo, ikiwa kesho ndiyo siku ya mwisho wa agizo hilo, Chalamila amewatahadharisha wafugaji hao kuondoka mapema katika ranchi hizo kabla hatua za kisheria hazijachukuliwa.

**Hali hiyo inahatarisha afya na usalama wa wanyamapori katika hifadhi hiyo, pindi wanapoingiliana na mifugo ya wananchi.**

Chalamila alifikia hatua hiyo baada ya kupokea malalamiko kwa wawekezaji ambao wamekuwa wakilalamika kwamba wafugaji hao wamevamia mashamba yao wakiwa na mifugo ikiwamo ng'ombe na mbuzi.

"Nitasimamia agizo hili kuhakikisha hakuna mifugo yoyote kwenye Hifadhi ya Ruaha na maeneo mengine ya uwekezaji, msihoji ni kwa namna gani nitaondoa ila mtakiona Alhamisi," alisema Chalamila.

Awali Mhifadhi Mwandamizi Hifadhi ya Taifa Ruaha, Sharif Abdul, alimweleza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, kuna wimbi kubwa la wafugaji ambao huingiza mifugo kwenye hifadhi hiyo.

Alisema hali hiyo inahatarisha afya na usalama wa wanyamapori katika hifadhi hiyo, pindi wanapoingiliana na mifugo ya wananchi.

Aliongeza wamekaa vikao vya kujadili tatizo hilo mara tatu ikiwajumuisha viongozi wa vijiji pamoja na wafugaji, lakini hakuna suluhisho lolote.

Katibu Mkuu wa Chama cha Wafugaji Tanzania, Matagili Mbigili, aliahidi kutekeleza agizo la Mkuu wa Mkoa kuondosha mifugo kwenye maeneo ya uwekezaji na hifadhi, huku akiwaomba wafugaji kuacha tabia hiyo.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akizungumza na wafugaji, wakulima na wawekezaji wa Bonde la Usangu, wilayani Mbarali, mkoani Mbeya jana. **PICHA GRACE MWAKALINGA**

# Wazee waomba dawa kuongezwa hospitalini

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAZEE kutoka Kata ya Rujewa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wameiomba serikali kupitia Wizara ya Afya kuongeza kasi ya upatikanaji wa dawa hospitalini kwenye madirisha maalum yaliyotengwa kwa ajili yao.

Wamesema kwa kufanya hivyo watakuwa na uhakika wa kupata matibabu, kuliko hivi sasa wanavyokosa dawa.

Katibu wa wazee Rujewa, Christina Mwalyaje, aliyasema hayo kwa niaba ya wazee wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wazee iliyoadhimishwa katika Kata ya Rujewa.

Walisema wanapofika kwenye vituo vya kutolewa huduma za afya, wahudumu hudai dawa zimekwisha hivyo wakanunue kwenye maduka, hali ya kuwa baadhi yao hawana uwezo wa kumudu gharama za kununua.

Kutokana na hali hiyo, wazee hao waliiomba ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya, kumteuwa mtu maalum ambaye atashughulikia suala hilo, ili kuwasaidia kupata matibabu ya uhakika.

Pia walitaka mtu huyo ahakikishe anaweka utaratibu wa kupunguza foleni na milolongo mingine ili watibiwe haraka.

Mwalyaje alisema moja ya vikwazo wanavyokabiliana navyo wazee ni pamoja na baadhi ya wagonjwa wengine kutumia dirisha hilo kupata matibabu.

"Naamini suala la upatikanaji wa dawa likishughulikiwa kwa ufanisi, wakaweka utaratibu wa utoaji huduma hakika afya zetu sisi wazee zitaimarika jambo la msingi ni kuwaomba watendaji wanaotoa huduma za afya kutomwangusha rais wetu kwa sababu amewekeza fedha nyingi," alisema Mwalyaje.

Akizungumzia suala La uwakilishi wa wazee kwenye vikao vya maamuzi, Mwalyaje aliomba wazee washirikishwe kwenye vikao vya mbalimbali vya maamuzi.

Miongoni mwa wazee hao, akiwamo Juma Michael. alisema kundi hilo linapaswa kuangaliwa kwa jicho la kipekee kwa sababu wanamchango mkubwa katika kulileta maendeleo taifa la Tanzania.

Alisema miongoni mwa masuala yanayotakiwa kuboreshwa ni uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya na maji kwa sababu ni maeneo yanayogusa maisha ya watu moja kwa moja.

Aidha, alitoa ushauri kwa serikali kuwa sera ya wazee ya mwaka 2003 itungiwe sheria ili wazee wapewe kutunzwa kama sera ilivyoandikwa.

## Waziri aagiza wawekezaji wenye madeni wapokwe ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameiagiza Bodi ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kunyang'anya ranchi zote zilizokodiwa na wawekezaji ambao wameshindwa kulipa madeni.

Alitoa agizo hilo akiwa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya wakati akizungumza na wakulima pamoja na wafugaji wa bonde la Usangu.

Alisema serikali inahitaji wamilikiwa wa ranchi zote walipe madeni yote kuanzia Januari 12 hadi Februari 15, majira ya saa saba mchana, kwamba zitakazoshindwa kulipa zinyang'anywe na kupewa wawekezaji wengine.

Aidha, alipiga marufuku kufanyika kwa shughuli za kilimo kwenye maeneo ya ranchi kwa madai kuwa ni kwenda kinyume na makubaliano ya mkataba.

"Nimetoa muda wa kuanzia Januari 12 hadi Februari 15 majira ya saa saba mchana Bodi ya NARCO iwe imekusanya madeni yote wanayodaiwa kwenye ranchi mbalimbali nchini, lakini wawekezaji kufuata makubaliano ya mikataba ili kila upande unufaike na ranchi hizo," alisema Waziri Ndaki.

Katika hatua nyingine aliwahakikishia wawekezaji wa ranchi mbalimbali nchini kwamba serikali imewaandalia mazingira mazuri ya kufanya shughuli zao na kuomba waendelee kushirikiana.

Katibu wa Wizara hiyo, Profesa Gabriel Ole Sante, aliwaomba wamiliki wa ranchi kutumia maeneo hayo kwa ajili ya mifugo na shughuli zingine ambazo ni kinyume na makubaliano.

Baadhi ya wakulima wa bonde la Usangu walioomba serikali kuwagawia eneo kwa ajili ya kilimo kuliko ilivyo sasa, ambapo wanakodishwa kwa gharama kubwa.

Ulia Mahenge aliiomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvivu kupewa eneo kwa ajili ya kilimo na kwamba yuko tayari kulipia gharama za vitalu.

Juzi, mwekezaji wa ranchi ya Usangu, Basil Mramba alimwakikishia Waziri Ndaki kulipa madeni yote ndani ya muda uliopangwa.

Alipongeza hatua ya Waziri Ndaki kutembelea eneo lake ambalo lina ukubwa wa hekta 43,727 ambao amefuga ng'ombe 531.



# RC aita wadau shida upatikanaji wa maji

**Na Hawa Aabdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa Mjini Magharibi, Idrissa Kitwana Mustafa, amesema watashirikiana na taasisi za ndani ya nchi kutatua kero zinazowakabili wananchi, ikiwamo ya upatikanaji wa majisafi na salama.

Kitwana alitoa ahadi hiyo wakati akizindua kisima cha majisafi na salama katika Shule ya Msingi Muungano, kilichojengwa kwa ufadhili wa Taasisi ya Al- Amin Relief katika Shehia ya Muungano, Wilaya ya Mjini Unguja.

Alisema kutokana na umuhimu wa huduma hiyo kwa jamii, lazima serikali ishirikiane kwa karibu na wadau mbalimbali kusaidia wananchi kuimarisha ustawi wa jamii.

"Ninatumia nafasi hii kupongeza uongozi wa Al- Amin kwa uamuzi wenu wa kusaidia huduma hii ya maji katika shule yetu, hatua ambayo inaonyesha moja kwa moja kuunga mkono jitihada za serikali za kuwaletea maendeleo wananchi wake," alisema.

Mkuu wa Mkoa alizitaka taasisi mbalimbali na wananchi wenye nia ya kuchimba visima, kufuata taratibu na sheria za Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), ili kuepuka madhara kwa jamii.

"Ninaomba niwakumbushe kwamba tunapotaka kusaidia jamii katika masuala ya maji, lazima tupate ushauri wa kitaalamu kutoka mamlaka husika, ili huduma hii iwe safi, lakini salama kwa afya zetu," aliagiza.

Mwalimu wa Shule hiyo, Zawadi Saleh Ali, alisema ujenzi wa kisima hicho, utaongeza ufanisi wa kazi na kuleta maendeleo zaidi kwa kuwa suala la ukosefu wa maji lilikuwa tatizo la muda mrefu kwao.

"Shule yetu ilikuwa na tatizo la ukosefu wa maji kwa muda mrefu, hatua ambayo ilikuwa ikirudisha nyuma jitihada zetu za utoji wa elimu kwa wanafunzi wetu," alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Al – Amin Relief, Abdulhamid Shaali Makame, alisema taasisi yao imekuwa ikijisaidia jamii katika sekta mbalimbali.

Alisema kwa sasa taasisi hiyo imeanzisha mpango maalum wa kusaidia wanawake wajane na watoto yatima katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar na kuomba uongozi wa serikali kuwasaidia kupata wafadhili kwa kuwa taasisi yao inategemea misaada kutoka kwa wahisani.

Ofisa Elimu wa Manispaa ya Mjini, Ali Omar Ali, aliushukuru uongozi wa taasisi hiyo kwa msaada huo na kuahidi kukitunza kisima hicho ili kitoe huduma kwa muda mrefu, ujenzi wake ukigharimu Sh. milioni nne.

# Dk. Mwinyi: Fedha sherehe za Mapinduzi zipelekwe elimu, afya

**Na Hawa Aabdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameagiza fedha za sherehe ya maadhimisho ya Miaka 57 ya Mpinduzi ya Zanzibar, zielekezwe katika kuboresha huduma za kijamii ikiwamo elimu na afya.

Dk. Mwinyi alitoa agizo hilo jana, katika hafla ya kuadhimisha miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye Viwanja vya Mnazimmoja, alipopokea maandamano yaliyofanywa na vikosi vya ulinzi na usalama na vyama vya kisiasa.

Alisema fedha ambazo zilipangwa kutumika katika sherehe hizo, ni vyema zikaelekezwa katika huduma muhimu kutokana na hali ya uchumi iliopo hivi sasa.

"Kwa kuwa hizi ni sherehe zangu za kwanza nikiwa Rais wa awamu ya nane, nilitamani sana kufanya sherehe za aina yake, lakini hali ya kiuchumi imechangia sherehe zetu mwaka huu kuzifanya katika utaratibu tofauti na ilivyozoeleka," alisema.

**Wakati umefika wa kuhangaika na uchumi wa mapinduzi kama ilivyokusudiwa katika sekta mbalimbali ikiwamo afya na kwa kutoa huduma bora katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar na kutoa elimu bora kwa wanafunzi nchini.**

Dk. Mwinyi aliwataka Wazanzibar kuyalinda Mapinduzi kwa kuleta maendeleo kama yalivyokusudiwa na Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume.

Alisema wakati umefika wa kuhangaika na uchumi wa mapinduzi kama ilivyokusudiwa katika sekta mbalimbali ikiwamo afya na kwa kutoa huduma bora katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar na kutoa elimu bora kwa wanafunzi nchini.

Alisema serikali yake pia inakusudia kuleta mapinduzi sekta ya kilimo, ili wakulima wa Zanzibar walime mazao yenye tija na kuondoa utegemezi wa kuagiza chakula kutoka nje ya nchi.

Dk. Mwinyi pia alisema wanakusudia kuleta mapinduzi katika sekta ya uvuvi ili wavuvi wavue kwa dhana za kisasa na kufaidika na bahari kuu. Dk. Mwinyi alisisitiza watumishi wa umma kujenga uwajibikaji na serikali kuboresha huduma na maslahi yao.

Alisema sekta ya sanaa na michezo itapewa kipaumbele ili wasanii na wanamichezo wafanye kazi zao kwa ufanisi na kutengeneza ajira kupitia sekta hiyo.

Dk. Mwinyi alikemea udhalilishaji wa kijinsia visiwani Zanzibar, akisisitiza umekuwa ukitia doa na aliagiza wahusika wote wa jinai hiyo kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo na kuachana na muhari.

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa, kisiasa na viongozi wakuu wastaafu.

Viongozi hao ni pamoja na Makamu wa Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, marais wastaafu wa Zanzibar: Dk. Ali Mohamed Shein; Amani abeid Amani Karume, Dk. Mohammed Gharib Bilali, Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman na Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharif Hamad.

Sherehe hizo pia zilipambwa na shangwe za wafuasi wa vyama vya siasa ikiwamo Chama Cha Mapinduzi (CCM) na ACT-Wazalendo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akihutubia wananchi wakati wa sherehe za kilele cha maadhimisho ya miaka 57 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# RC aita wadau shida upatikanaji maji

**Na Hawa Aabdallah,** ZANZIBAR

KAMPUNI ya Kimataifa ya Semcrete ya Misri, inayojihusisha na miundombinu na uwekezaji katika miradi ya bandari, barabara, afya, maji, elimu na umeme, imeonyesha utayari kuwekeza visiwani Zanzibar.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo, Sherif Nazmy, alibainisha kusudio lao hilo wakati ujumbe aliouongoza upofanya mazungumao na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ofisini kwake Vuga mjini Zanzibar.

Nazmy alisema kutokana na mazingira rafiki ya uwekezaji yanayokwenda sambamba na ukarimu wa watu wa Zanzibar, uongozi wa Samcrete uko tayari kuanzia sasa kuwekeza katika mradi utakaochaguliwa kwa awamu ya mwanzo.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina fursa ya kuchagua miundombinu yoyote ambayo kampuni yetu itakuwa tayari kuanza nayo katika mwelekeo wa kuzitumia fursa za uwekezaji," alisema.

Mkurugenzi huyo alimweleza Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwamba, kampuni yao inalenga kuimarisha ustawi wa wananchi wa Zanzibar.

Sherf Sabry, mmoja wa maofisa wa ngazi za juu katika kampuni hiyo, alisema kampuni yao iko tayari kutoa utaalamu na fedha kukamilisha mradi wowote utakaokubaliana.

Sabri alisema Kampuni ya Semcrete tayari imeshajipatia uzoefu wa kutosha kwa miaka mingi, ikiendelea kusambaa katika pembe mbalimbali za dunia.

Akitoa shukrani zake kwa kampuni hiyo, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Abdulla, alisema serikali imejizatiti kuhakikisha kunakuwa na uwekezaji wenye tija.

Ndani ya mazungumzo yao, kiongozi huyo wa serikali alilazimika kuwasiliana moja kwa moja kwa njia ya simu na Waziri anayesimamia masuala ya Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, Mudrik Suleiman Soraga, akimwagiza kukutana na uongozi wa kampuni hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano : 0713327613.

## ANATAFUTWA DEREVA

Anatafutwa dereva wa kike mwenye uzoefu wa kuendesha Magari Mjini Dar es Salaam. Mwenye nia na kazi hiyo apige namba 0784691605/0715691605.

## OFISI ZA MATANGAZO

Mikocheni Industial Area,
Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

---

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA KIGOMA**

..............................KIGOMA..................
.......................................................
MAHALI................KIGOMA..................
.......................................................
.......................................................
MAOMBI NAMBA ........................53 YA
MWKA 2019...................................
JUMANNE HUSSSEIN K. JUMANNE CHULEHA
.........................MWOMBAJI.
DHIDI YA
SULEMMANI ANTONY
.................MJIBU MAOMBI

**WITO KUITWA SHAURINI**

KWA SULEIMAN ANTONY
Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa /kusikili zwa tarehe 18 mwezi wa 01 mwaka 2021 asubuhi /mchana mbele ya muheshimiwa F Chinuku Mwenyekiti wa baraza.Hivyo unaamriwa kuhudhulia mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 9 mwezi wa 11 mwaka 2020

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KAHAMA**
**WILAYANI YA KAHAMA**
**CIVIL CASE 86/2020**

ALISSAR COMPAY LIMITED........PLAINTIFF
DHIDI YA
TOHANA JUMA NYAMTIMBA........DEFENDANT
KUITWA SHAURINI

**KWA: YOHANA JUMA NYAMTIMBA**
**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake hapa Mahakama ya Wilaya ya Kahama katika shauri tajwa hapo juu,ambalo litatajwa tarehe 19/1/2021.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya mahakama hii mnamo tarehe 19/1/2021,saa 2:30 asubuhi bila kukosa au kuchelewa, siku hiyo ni siku ya kutajwa kwa shauri hilo ni lazima kuleta utetezi wako na Hati zote zinazohusu shauri hilo ili kujibu maombi katika shauri hilo.
Fahamu kuwa usipohudhuria siku hiyo, shauri laweza kuendelea kusikilizwa na kutolewa hukumu upande mmoja bila wewe kuwepo.
Imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya Mahakama hii leo tarehe 08 Mwezi Januari mwaka 2021.

C.L,Chovenye
HAKIMU MKAZI WILAYA
KAHAMA

---

**IN THE DISTRICT COURT OF MPWAPWA**
**AT MPWAPWA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 1 of 2021**

In the matter of the Estate of the Late
**JOYCE ZEBEDAYO MAZENGO**
And
In the matter of Petitioner for letters administrating by
**RENATUS MAZENGO LENDO**

**GENERAL CITATION**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the late **JOYCE ZEBEDAYO MAZENGO** (Deceased) hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the Petitioner **RENATUS MAZENGO LENDO**. Objections in the grant should filed on or before the 26 day of January, 2021.
Dated at Mpwapwa this 06 day of January, 2021.

---

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku




OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wanajeshi wadaiwa kuvamia makazi ya Bobi Wine

**Kampala, UGANDA**

MGOMBEA wa urais nchini Uganda, Robert Kyagulanyi maarufu 'Bobi Wine', amekatiza mahojiano yake redioni, baada ya wanajeshi kuvamia nyumba yake mjini Kampala.

Vyombo vya habari nchini Uganda vinaripoti kuwa leo asubuhi wanajeshi walizingira nyumba yake na kuwakamata walinzi wake wote na wote waliokuwa katika eneo la makazi ya mwanasiasa huyo wa upinzani.

Hata hivyo hakuna sababu iliyotolewa juu ya uvamizi huo.

Bobi Wine, alikuwa akihojiwa katika kipindi cha redio kiitwacho Kenya HOT 96 cha kila asubuhi, na kusema kuwa anawaona maofisa wa kijeshi wakiwapiga walinzi wa usalama wake.

Sauti zilisikika kwa mbali kupitia redio wakati wa tukio hilo, kabla ya Bobi Wine kukata simu ya mahojiano.

Wakati hayo yakijiri, Rais Yoweri Museveni, ambaye anawania muhula wa sita madarakani, alitarajiwa kulihutubia taifa jana, kupitia vyombo vya habari vya kitaifa.

Waganda wanatarajia kufanya uchaguzi wa wabunge na urais kesho.

Kampeni za uchaguzi nchini Uganda, zimekuwa zikigubikwa na ghasia zilizosababisha mauaji. ***BBC***

# Israel kujenga nyumba 850 ukingo wa magharibi makazi ya Wapalestina

**Jerusalem, ISRAEL**

IMEELEZWA kuwa Israeli, itajenga kinyume cha sheria nyumba 850 kwa walowezi wa Kiyahudi katika Ukingo wa Magharibi, uliokaliwa kimabavu.

Mamlaka ya Israel, imeidhinisha uamuzi wa kujenga makazi mengine 850 katika Ukingo wa Magharibi kwa ajili ya walowezi wa Kiyahudi wiki ijayo.

Taarifa hiyo ni kulingana na Shirika la Utangazaji la Umma la Israel (KAN).

Katika ripoti hiyo, imebainika kuwa Waziri wa Ulinzi wa Israel, Benny Gantz, aliagiza Baraza la Mipango ya Juu la Kitengo cha Utawala wa Kiraia Ndani ya Kitengo cha Uratibu wa Shughuli za Serikali (COGAT), kujenga nyumba zaidi eneo hilo.

Hakuna taarifa rasmi, iliyotolewa kutoka mamlaka ya Israel juu ya suala hilo.

Inafahamika kuwa, Israel imechukua hatua kama hiyo muda mfupi kabla ya Rais mteule, Joe Biden, kuchukua wadhifa wake. ***TRT***



Jengo la Capitol eneo linalotarajiwa Rais mteule, Joe Biden na Makamu wa Rais, Kamala Harris, kula kiapo wiki ijayo. Usalama umeimarishwa kuelekea hafla hiyo kufuatia wiki iliyopita wafuasi wa Rais Donald Trump, kuvamia eneo hilo na kusababisha vifo. **PICHA/REUTERS**

## Bajeti yatia fora ununuzi wa maua Ikulu ya Ufaransa

**Paris, UFARANSA**

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, ametenga bajeti ya fedha ya euro 600,000 kwa ajili ya maua ya Ikulu ya Elysee.

Fedha hizo, ni kwa ajili ya maua ya mkewe, Brigitte Macron katika Ikulu ya Elysee, umezua utata katika vyombo vya habari vya Kifaransa.

Kulingana na taarifa kutoka Shirika la Utangazaji la kisiasa la Kifaransa la Politis, iliarifiwa kwamba Macron na mkewe walitumia euro 600,000 kwa ajili ya maua katika Jumba la Ikulu ya Elysee.

Elysee ni makao makuu rasmi ya rais katika mji mkuu wa Paris.

Matumizi kama hayo yalitafsiriwa kama aibu kwa umma wa Ufaransa, wakati nchi hiyo ilikuwa ikijitahidi kupata ahueni, kutokana na mzigo wa kifedha uliotumika kwa ajili ya janga la corona.

Serikali ya Macron, ilikuwa imeahidi kutenga euro bilioni 100, ili kuharakisha mchakato wa kufufua uchumi wa nchi.

Baada ya taarifa hiyo, wananchi wa Ufaransa walidhihirisha hisia na maoni yao kwenye mitandao ya kijamii.

Mmoja wa watumiaji wa mitandao ya kijamii alisema, "Tunahimizwa kulinda pesa zetu, tunatozwa ushuru zaidi na yeye anajifurahisha."

Hii inamaanisha kuwa bajeti za maua ni karibu mara tano zaidi, kuliko zile za marais waliotangulia ambao ni Francois Hollande na Nicolas Sarkozy.

Bajeti ya maua pia ilibainika kuongezeka haraka wakati wa Ikulu ya Elysee ilipofungwa kwa umma na mapokezi machache yaliyofanyika kutokana na vizuizi vya Covid-19.

Septemba, mwaka jana, ilitangazwa ukarabati wa chumba cha Dhahabu cha Elysee, uligharimu euro 927,000.

Ikulu hiyo, gazeti la Le Canard Enchaine, lilitangaza kwamba imenunua sahani mpya zenye thamani ya euro 498,000.

Ikulu ya Elysee, ilipinga kiwango hicho cha fedha na kusema kuwa bei ilikuwa karibu na fedha euro 49,000. ***TRT***

# FBI yahofia usalama Biden, Kamala wakijiandaa kuapa wiki ijayo

**Washington, MAREKANI**

IDARA ya upelelezi nchini Marekani (FBI), inaonya kuwa huenda kukashuhudiwa maandamano yenye ghasia nchini humo, kuelekea kuapishwa kwa rais mteule na makamu wa rais.

FBI inasema katika ripoti yake kuwa, kuna makundi yenye silaha yanayopanga maandamano hayo yenye fujo katika majimbo yote 50 nchini humo.

Idara hiyo ilifafanua inatokana na kukaribia siku ya kuapishwa kwa Joe Biden na Kamala Harris, Januari, 20, mwaka huu.

Ripoti ya FBI, imezua wasiwasi wa usalama kuelekea shughuli za kula kiapo zitakazofanyika katika eneo la Capitol Hill.

Biden alisema haogopi kuapishwa katika eneo hilo, ambalo lilishuhuhudia vurugu wiki iliyopita, baada ya wafuasi wa rais anayeondoka madarakani, Donald Trump, kuvamia majengo ya bunge la Congress na lile la wawakilishi kujaribu kuzuia kuidhinishwa kwa ushindi wa Biden.

Wakati hayo yakijiri, Trump alitangaza hali ya hatari katika jiji kuu Washington na kuamuru usalama kuimarishwa, wakati Kaimu Waziri wa Usalama wa Ndani, Chad Wolf, akijiuzulu na kufikisha idadi ya mawaziri waliojiuzulu katika serikali ya Trump tangu kuzuka kwa fujo hizo, kufikia watatu. ***RFI***



# LUKAKU ANA NGUVU ZA ASILI

**MILAN, Italia**

KIUNGO wa Inter Milan, Nicolo Barella, amesema wanahitajika wachezaji wawili au watatu kuweza kumzuia Romelu Lukaku kwa sababu nyota huyu ni "Nguvu ya Asili".

Kiungo huyu amefanikiwa kuweka wavuni mabao 12 kwenye mechi 16 za Serie A msimu huu na amewasaidia Inter kuwa nafasi ya pili baada ya mechi 17 za ligi.

Barella, nyota wa kimataifa wa Italia, alizungumzia kasi na nguvu za mwili wa straika huyo wa kati huku akimsifu Mbelgiji huyo.

Lukaku amechangia mabao 50 na pasi za mwisho tisa katika michezo 72 tangu kuhamia kwake akitokea Manchester United.

"Lukaku na Shaquille O'Neal hufanya nguvu ya mwili kuwa nguzo yao kubwa, Lakini Romelu pia ni zaidi," alisema Barella akinukuliwa na Sky Sport Italia.

"Hata kwenye mazoezi, tunahitaji wachezaji wawili au watatu kumzuia. Yeye ni nguvu ya asili."

## UPAMECANO MLANGO WAZI KUONDOKA LEIPZIG

**LEIPZIG, Ujerumani**

RB Leipzig wamefungua milango yao kwa beki kisiki, Dayot Upamecano kuondoka klabuni hapo.

Upamecano ni miongoni mwa walinzi wanaotajwa kama lulu kwenye soka la Ulaya kwa sasa.

Akiwa na umri wa miaka 22, anawindwa na timu kadhaa barani Ulaya ikiwamo Manchester United, Liverpool na Chelsea.

Japokuwa usajili wa Upamecano kwenye dirisha la usajili la Januari hii hauonekani, mchezaji huyo raia wa Ufaransa ataweza kuondoka Leipzig kuanzia Julai, na ili kumtoa Ujerumani, timu yoyote itakayosogelea milango ya Leipzig iwe na dau la pauni milioni 40.

Mkurugenzi wa Leipzig, Oliver Mintzlaff amesema. "Tuna kikosi ambacho kimejaa ubora kwenye kila nafasi, kwa hiyo tutauza baadhi ya wachezaji wazuri kama itakuwa na faida ya kiuchumi.

"Na tutaendelea kuuza pale tu tutakapoona inafaa na si kwa sababu mchezaji fulani anatakiwa sehemu basi sisi tutamto tu kirahisi.

Nyota huyo amekuwa akiwindwa sana na klabu kubwa na sasa ni wazi kwamba majaliwa yake nchini Ujerumani yako shakani, kwani anaweza kuondoka wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho.

## DYBALA KUKOSA MECHI MUHIMU ZA JUVENTUS

**TURIN, Italia**



PAULO Dybala atazikosa mechi muhimu za Juventus za Januari hii dhidi ya Inter Milan na Napoli, huku kukiwa na changamoto za kupata mbadala wake kutoka kikosi cha vijana wa chini ya umri wa miaka 23.

Kikosi hicho kwa sasa kimewekwa karantini baada ya visa vitatu vya maambukizi ya virusi vya corona.

Dybala alipata jeraha la goti kwenye mechi dhidi ya Sassuolo Jumapili, na taarifa ya kitabibu inaonekana bado ana shida kidogo kumkwamisha kuingia dimbani.

Staa huyu wa Argentina anatarajiwa kuwa atakuwa nje ya dimba kwa takribani siku 15 hadi 20, ikiwa inamaanisha kuwa nyota huyu atalazimika kuzikosa mechi dhidi ya Inter na Napoli.

Juventus wanasafiri kwenda San Siro kwenye mechi dhidi ya Nerazurri, wakati watakutana na Napoli pale dimba la Mapei kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Italia Supercup Januari 20.

Dybala ataendelea kuuguza jeraha lake na kwa mujibu wa taarifa za kitabibu anaweza kuanza kurejea katika hali yake taratibu angalau baada ya siku 15.

## HABARI MICHEZO

# SANCHO:
## MAMBO MAGUMU KWANGU



**DORTMUND, Ujerumani**

WINGA wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 20, amekiri kwamba amekuwa na msimu mbaya yeye binafsi, hasa baada ya tetesi kumhusisha kujiunga na Manchester United.

Sancho alifunga mabao 17 kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na kuisaidia Dortmund kushika nafasi ya pili katika msimamo wa msimu wa 2019-20, hivyo kujiweka katika nafasi ya mchezaji mdogo mwenye gharama zaidi.

Man United walijaribu kumsajili mchezaji huyo katika majira ya kiangazi, lakini ilishindikana baada ya kushindwa kufikia dau la euro milioni 100 zilizokuwa zinatakiwa na Dortmund, katika mazungumzo yaliyodumu kwa mwezi mzima.

"Ni wazi msimu huu umekuwa mgumu sana kwangu binafsi," alisema mchezaji huyo katika tovuti ya BVB.

"Kwa hivyo nilijua nilipokwenda, nilizingatia tu mchezo wangu na nikarudi nikitamani kwenda.

"Ninafanya kazi kwa bidii kila siku kwenye mazoezi na uwanjani kwa hivyo ninafurahi kupata mabao na kutoa pasi za mwisho."

# WACHEZAJI KUJILIPIA WAKIPATA CORONA

**LONDON, England**

WAKATI dunia ikiendelea kupambana na mlipuko wa virusi vya corona, Ligi Kuu England (EPL), itaweka kipengele cha Covid-19 kwenye mikataba ya wachezaji.

Klabu za EPL na EFL zinajaribu kuhakikisha kunakuwa na kipengele cha kisheria kwenye mikataba ya wachezaji (wapya na waliopo), ambacho kitawataka kujigharamia kama Covid-19 itaendelea kuwa changamoto na mashabiki wakiendelea kuzuiwa kuingia viwanjani.

Kupitia Sky Sports, imeripotiwa kuwa mikataba mingi ya usajili wa mkopo imejumuisha kipengele cha Covid-19 na kwamba usajili unaweza kusitishwa endapo hali itazidi kuwa mbaya na kuharibu msimu mzima wa soka.

Sambamba na kipengele hicho, klabu pia zinajitahidi kuhakikisha kunakuwa na msimamo wa kisheria kwenye suala la kupunguza mishahara ya wachezaji kama mchezo wa soka utaendelea kuchezwa bila mashabiki kuanzia msimu ujao na kuendelea.

Uwapo wa vipengele hivi unasababisha majadiliano kati ya klabu na wachezaji kuwa magumu zaidi kuliko ilivyowahi kuwa hapo awali.



# LIVERPOOL KUMTOA DEN BERG KWA MKOPO

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL imefanya mazungumzo na klabu tatu kuhusu uwezekano wa uhamisho wa mkopo kwa beki mchanga, Sepp van den Berg.

Wekundu hao wanamtaka kijana huyo wa miaka 19 kupata uzoefu wa kikosi cha kwanza, na kwa hivyo watamruhusu aondoke mwezi huu licha ya ukosefu wa chaguzi za klabu katika beki ya kati.

Majadiliano tayari yamefanyika na klabu za nchini Ubelgiji, Ujerumani na Uswisi, na kwa mujibu wa Goal.com makubaliano yanaweza kumalizika wiki hii.

Van den Berg alihamia pale Merseyside kutoka PEC Zwolle Juni 2019, na Liverpool ililipa pauni milioni 1.3 kupata huduma yake.

Tangu wakati huo amecheza mechi nne za kikosi hicho cha Jurgen Klopp, zote zikiwa kwenye mashindano ya kombe la ndani, lakini hajaonekana kabisa kwenye kikosi cha kwanza msimu huu licha ya shida za majeraha za mabingwa hao wa Ligi Kuu England.

Uamuzi wa mwisho sasa utafanywa, na Liverpool inataka kuhakikisha Van den Berg ana nafasi ya kucheza michezo ya kawaida kwa kiwango ambacho kitamruhusu kukuza maeneo muhimu ya mchezo wake.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER AVUTIWA NA MBIO UBINGWA EPL

●●●Kwa upande wangu, inavutia, kwa mashabiki ndio inafurahisha zaidi, kwa namna yoyote kila...

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema anafurahishwa sana na mbio za wazi za ubingwa wa Ligi Kuu ya England (EPL), msimu huu, wakati 'Mashetani Wekundu' hao wakisaka taji.

United jana Jumanne ilikuwa ikicheza na Burnley huku wakiwa pointi sawa, 33, na bingwa mtetezi Liverpool kileleni mwa msimamo na wana nafasi ya kupaa zaidi kwa sababu wana mchezo mmoja mkononi.

Liverpool ilitwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu uliopita kwa kuongoza kwa pointi 18 kileleni mwa msimamo, lakini kwa sasa wamewapita pointi moja tu Leicester City wanaoshika nafasi ya tatu, huku Chelsea wakipitwa saba baada ya kushuka dimbani mara 17.

Solskjaer ana amini United imeonyesha ushindani mkubwa katika mbio za kuwania taji lake la kwanza la Ligi Kuu tangu msimu wa 2012-13.

"Nafikiri timu zote zinataka kuchukua pointi kwenye Ligi Kuu, bila shaka yoyote," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini nafikiri ni aina ya msimu wenyewe, aina ya mwaka, aina ya hali halisi ambapo kumekuwa na kupanda na kushuka, kutokuwa na matokeo mazuri mfululizo na kiwango cha kuvutia.

"Kwa upande wangu mimi, inavutia. Kwa mashabiki ndio inafurahisha zaidi, kwa namna yoyote kila mmoja anafurahia zaidi msimu huu tofauti na msimu uliopita.

"Umekuwa na mambo mengi, lakini sasa tunasahau na kuendelea na ratiba zetu kama kawaida, ingawa mambo yalianza kwa ugumu sana."

## KWA UFUPI

**SPURS KUMSAJILI MILITAO**

TOTTENHAM Hotspur huenda ikamsajili kwa mkopo mlinzi wa Brazil, Eder Militao, mwenye umri wa miaka 22, anayesakwa na AS Roma, AC Milan na Inter Milan kutoka Real Madrid kukiwa na kipengele cha kumnunua kwa mkataba wa kudumu. ***(Corriere dello Sport)***

**MOURINHO AMTAKA GONZALEZ**

JOSE Mourinho ameiingiza Tottenham Hotspur kwenye mbio moja na Leeds pamoja na Juventus katika kumsaka winga wa klabu ya Stuttgart, Nicolas Gonzalez, mwenye umri wa miaka 22, huku mchezaji huyo wa Argentina akilengwa katika dirisha la uhamisho la kipindi cha majira ya joto kijacho. ***(The Athletic)***

**WINKS ATAKIWA VALENCIA**

KLABU ya Valencia inawania kumsajili kiungo wa kati wa Tottenham Hotspur, Harry Winks, mwenye umri wa miaka 24 kwa mkopo. ***(Football London)***

**BRIGHTON YAIPIKU NEWCASTLE**

KLABU ya Brighton ina imani kuwa wameishinda Newcastle United katika mbio za kumsajili kiungo wa kati wa Ecuador, Moises Caicedo, kutoka klabu ya Indipendiente del Valle. Kinda huyo mwenye umri wa miaka 19, alikuwa akilengwa na klabu ya Manchester United. ***(Talksport)***

**N'ZONZI AHUSISHWA ARSENAL**

KIUNGO wa Ufaransa na mshindi wa Kombe la Dunia, Steven N'Zonzi, huenda mkataba wake wa mkopo katika klabu ya Rennes ukakatishwa baada ya kuhusishwa na uhamisho wa kwenda Arsenal na Everton. ***(Foot Mercato)***

**DEMBELE HUYO ATLETICO**

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa na Lyon, Moussa Dembele, mwenye umri wa miaka 24, anakaribia kukamilisha uhamisho wa kuelekea Atletico Madrid baada ya kukataa kwenda West Ham. ***(Telefoot via Sky Sports)***

**BAKAYOKO KUBAKI NAPOLI**

NYOTA wa Chelsea, Tiemoue Bakayoko, anatarajiwa kuondoka moja kwa moja katika klabu hiyo ya Stamford Bridge, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, akitaka kubaki Napoli ambapo anacheza kwa mkopo. ***(Star)***

**WILLMES KURUDI NEWCASTLE**

MLINZI wa Uholanzi, Jetro Willems mwenye umri wa miaka 26, anaonekana huenda akarudi katika klabu ya Newcastle United kutoka Eintracht Frankfurt. ***(Chronicle)***

**LEEDS WAMTAKA BJORKAN**

KLABU ya Leeds United imehusishwa na beki wa Norway anayetafutwa sana na Sampdoria mwenye umri wa miaka 22, Fredrik Andre Bjorkan. ***(La Repubblica via Yorkshire Evening Post)***

**ARSENAL KUMTOSA BUENDIA**

ARSENAL haina tena mpango wa kumsajili kiungo wa kati wa Norwich, Emi Buendia, baada ya klabu hiyo kuweka dau la pauni milioni 40 ili kumwachia mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina. ***(Express)***

**BURNLEY WAJITOSA KWA KENNY**

KLABU ya Burnley inatarajiwa kuwasilisha ombi la kumsajili mlinzi wa Everton, Jonjoe Kenny, mwenye umri wa miaka 23, baada ya hapo awali kushindwa kumsajili nyota huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya England ya wachezaji chini ya umri wa miaka 21. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

# MOROCCO ATOA SABABU SIMBA KUITOA NAMUNGO

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kufurushwa nje na timu ya Simba katika hatua ya nusu fainali ya michuano ya Kombe la Mapinduzi juzi, Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, amesema makosa madogo waliyoyafanya pamoja na kucheza mechi mfululizo katika mashindano hayo ni miongoni mwa sababu zilizochangia kutolewa.

Aidha, Morocco alisema hii ni mara ya kwanza kwa Namungo kushiriki Kombe la Mapinduzi, hivyo kukosa uzoefu wa michuano hiyo pia ni sababu nyingine ya kutolewa na Simba baada ya juzi kukubali kipigo cha mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Amaan.

"Kama mwalimu sikufurahia matokeo hayo, lakini nawapongeza wachezaji kwa kujituma na kufanya vizuri pale walipopata nafasi za kufunga na hata kuokoa ila haikuwa bahati kwao.

"Wachezaji wamejituma, wameonyesha uwezo wa kufanya vizuri katika michezo yote tuliyocheza, naamini tutafanya vizuri zaidi katika michuano mingine na ijayo iwapo tutapata nafasi ya kushiriki," alisema.

Akizungumzia suala la waamuzi waliochezesha mchezo baada ya wachezaji wake kuonekana wakiwalalamikia mara kwa mara hususan mwamuzi wa kati, Mohamed Kassim, Morocco alisema walichezesha vizuri ila malalamiko hayo yalichangiwa na ugumu wa mchezo huo na kama kuna upungufu kidogo ni makosa ya kibinadamu ambayo ni kawaida kutokea mchezoni.

Kwa matokeo hayo, Simba itashuka dimba la Amaan leo saa 2:15 usiku dhidi ya Yanga katika mechi ya fainali baada ya watani zao hao wa jadi kuwatoa Azam FC kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 5-4 kutokana na dakika 90 za mchezo kumalizika zikiwa sare ya bao 1-1.

NAMILIKI...



Mchezaji wa timu ya JKT Queens, Zabela John (kulia), akimiliki mpira huku akipata upinzani mkali kutoka kwa mchezaji wa Ruvuma Queens, Swaumu Salum, kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake uliopigwa Uwanja wa Karume jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nyota wa majaribio Simba washindwa kutoboa

**Na Adam Fungamwango**

WACHEZAJI wapya walioletwa klabu ya Simba kufanya majaribio, ni kama tayari wameshindwa baada ya kushindwa kuonyesha ubora wao kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi, imeelezwa.

Wachezaji hao ni Benard Agele 'Coulibaly' kutoka Sudan Kusini, Kelvin Moyo na Ian Nyoni wote kutoka Zimbabwe, ambao wameshindwa kuwaridhisha mabosi wa klabu hiyo, benchi la ufundi na hata wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

Habari za ndani kutoka Zanzibar zinaeleza wachezaji hao ambao walishiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi inayomalizika leo kwenye fainali kati ya Simba na Yanga, wameonekana kutokidhi matakwa ya benchi la ufundi.

"Imeonekana kuwa viwango vyao ni vya kawaida sana, ni kama vya wachezaji tulionao tu kwenye klabu ya Simba na hata hapa Tanzania, kwa hiyo sidhani kama kuna hata mmoja atakayesajiliwa," kilieleza chanzo chetu.

Lakini Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Selemani Matola, aliwatetea akieleza wachezaji huko walikotoka ligi zao zimesimama kwa hiyo hawana utimamu wa mwili.

"Unajua wengi wa wachezaji wanaokuja kwa majaribio ligi zao kwenye nchi wanazotoka zimesimama kwa hiyo hawako fiti, hawana utimamu wa mwili kwa sasa. Hata mechi nilizowapa walikuwa wanalalamika misuli na mpaka sasa hawako vizuri sana, nikaona bora niwapumzishe kwenye mechi ya Namungo na kuwatumia zaidi wachezaji ambao wako tayari kucheza mashindano hayo.

Hata hivyo, Matola hakusema kama watasajiliwa au wataachwa, lakini taarifa zinadai kuwa wameonekana hawatoshi kuichezea klabu kama Simba inayotaka wachezaji ambao wako tayari kwa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Baadhi ya mashabiki wa klabu hiyo wameonyesha wasiwasi wao juu ya viwango vya wachezaji hao na kusema kuwa viongozi wanapaswa kuwa makini na wasisajili wachezaji wa majaribio.

## Miraji anukia Kiatu Mapinduzi Cup

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI michuano ya Kombe la Mapinduzi ikimalizika leo kwa Simba na Yanga kucheza fainali, straika wa 'Wekundu wa Msimbazi' hao, Miraji Athuman, ndiye anayeongoza katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu cha mashindano hayo.

Simba ambayo imetinga fainali kwa kuitoa Namungo FC kwenye mechi ya nusu fainali iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Amaan, inakutana na Yanga leo ambayo nayo juzi iliitoa Azam FC kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 5-4 baada ya sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90.

Hadi sasa kabla ya mechi ya leo, Miraji amecheka na nyavu mara nne kwenye michuano hiyo iliyoshirikisha timu tisa zikiwa katika makundi matatu mwaka huu huku Simba ikiwa Kundi B sambamba na Chipukizi ya Pemba na bingwa mtetezi, Mtibwa Sugar.

Miraji alianza kucheka na nyavu dhidi ya Chipukizi, akifunga mabao mawili Simba ikishinda 3-1 na kisha kutupia moja wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Mtibwa Sugar kabla ya juzi kuziona nyavu tena wakishinda 2-1 dhidi ya Namungo FC.

Mchezaji anayemfuata kwa karibu katika mbio hizo za kuwania ufungaji bora wa Kombe la Mapinduzi ni mshambuliaji mwenza wa Simba, Meddie Kagere pamoja na Steven Sey wa Namungo FC ambao kila mmoja amezifumania nyavu mara mbili.

## Manyara kupata viongozi Februari

**Na Shufaa Lyimo**

UCHAGUZI wa viongozi wa Chama cha Soka Mkoa wa Manyara (MARFA), unatarajiwa kufanyika Februari 12, mwaka huu, baada ya uongozi uliokuwapo mwanzo kutupiliwa mbali.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Michezo wa mkoa huo, Charles Maguzo, alisema mkoa huo umeshindwa kupata timu inayoshiriki Ligi Kuu kutokana na uongozi uliopita kukiuka sheria na taratibu za mpira.

Alisema uchaguzi wa awali ambao uongozi wao umetupiwa virago, ulifanyika kinyemela Septemba 5, mwaka jana, hivyo baada ya uchunguzi wamebaini kuwapo kwa kasoro nyingi hivyo kuamua kuuvunja na kutangaza kufanyika upya.

"Tumeshindwa kuwa na timu inayoshiriki Ligi Kuu kwa sababu ya uongozi uliokuwapo ulikuwa haushirikiani na wananchi wala walikuwa hawajui mapato yanapatikana kiasi gani, tukaitisha mkutano wetu kila mdau aliona dosari zilizokuwapo," alisema Charles.

Alisema kwa sasa wanaamini watapata viongozi waadilifu ambao wataleta maendeleo ya michezo katika mkoa wao huo na kwamba jana ndio walifunga mchakato wa kuchukua fomu za kugombea nafasi ya mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu mkuu na msaidizi wake, mweka hazina pamoja na mjumbe wa mkutano mkuu.

# Michezo

Jumatano Januari 13, 2021

Nipashe




## SOLSKJAER AVUTIWA NA MBIO UBINGWA EPL

HABARI UK 22

KWAHERI...




Wachezaji wa Taifa Stars (kulia) na DR Congo, wakimpa heshima kwa kumpigia makofi Aggrey Morris (anayepita katikati), wakati akiaga rasmi kutundika daluga la kuichezea Stars, kwenye mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana na timu hizo kutoka sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# SIMBA, YANGA FAINALI YA KIBABE MAPINDUZI

●●●Kuutapisha Uwanja wa Amaan leo, tambo zatawala kila mastaa waliobaki Dar waitwa...

**Na Saada Akida**

MIAMBA ya Ligi Kuu Bara na watani wa jadi nchini, Simba na Yanga, leo inashuka katika dimba la Amaan visiwani hapo, kwenye mechi ya fainali ya Kombe la Mapinduzi itakayoikutanisha katika hatua hiyo kwa mara ya pili tangu ilipoanza kufanyika kwa mara ya kwanza mwaka 2007.

Yanga ndiyo ilikuwa ya kwanza kulibeba taji hilo mwaka 2007, michuano hiyo ikifanyika kwa mara ya kwanza, lakini miamba hiyo ya Bara ilikutana kwa mara ya kwanza katika mechi ya fainali mwaka 2011 na Simba kulibeba taji hilo baada ya kuibuka na ushindi. Hata hivyo, leo timu hizo zinakutana, Simba ikiwania kulitwaa kwa mara ya nne wakati Yanga ikiwania kulibeba kombe hilo kwa mara ya pili.

Simba ililitwaa kwa mara ya kwanza mwaka 2008 baada ya kuifunga Mtibwa Sugar kwenye mechi ya fainali, kisha ikalibeba 2011 kwa kuichapa Yanga kabla ya kulinyanyua tena kombe hilo mwaka 2015 kwa kuifunga Mtibwa Sugar.

Wakati zikishuka dimbani leo, Azam FC waliotolewa na Yanga kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 5-4 juzi baada ya sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90, wanabaki kuwa mabingwa wa kihistoria wa michuano hiyo baada ya kulitwaa mara tano ikifuatiwa na Simba mara tatu na Mtibwa Sugar mara mbili, timu zingine zilizosalia, Yanga, Miembeni na URA, zimelibeba mara moja moja.

Hata hivyo, neno ushindi ndilo pekee linalotajwa na viongozi, makocha wa timu zote mbili, Yanga na Simba pamoja na mashabiki wa timu hizo kila mmoja akitamba timu yake kulitwaa leo katika mechi hiyo itakayopigwa majira ya saa 2:15 usiku.

Kuelekea fainali hiyo timu hizo mbili tayari zinaelezwa kuingia mchecheto wa ushindi huku zikiwaita wachezaji wao ambao walibaki jijini Dar es Salaam kwa sababu mbalimbali ikiwamo mapumziko.

Taarifa zilizolifikia gazeti hili zinaeleza nyota wa Simba akiwamo Luis Miqussoine, Clatous Chama na Rally Bwalya walitarajiwa kuungana na kikosi hicho jana jioni kwa ajili ya kuongeza nguvu katika fainali hiyo.

"Wanakuja leo (jana) kwa ndege tayari kuungana na wenzao, unajua mechi ya watani haina cha udogo wa mashindano, ukifungwa inaingia tu kwenye rekodi," alisema mtoa habari wetu, huku uongozi wa Simba ukikataa katu katu kuweka wazi kuhusu suala hilo.

Lakini kwa upande wa Yanga ambao nao kuna baadhi ya nyota akiwamo Said Ntibazonkiza, Lamine Moro nao wanaelezwa tayari wameungana na wenzao ikiwa ni pamoja na usajili mpya Dickson Job ambaye amesajiliwa juzi na Yanga akitokea Mtibwa Sugar.

Kocha Mkuu wa Yanga, Cedric Kaze, alisema baada ya kumaliza nusu fainali dhidi ya Azam FC wamejipanga kuwakabili Simba katika fainali hiyo, huku akieleza ataendelea kutumia wachezaji wake waliokuwapo tangu awali.

"Utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa kwa sababu ni fainali, kila mmoja anahitaji kupata matokeo mazuri kwa upande wetu, tumejiandaa kutwaa ubingwa huo licha ya kukosa baadhi ya nyota wangu," alisema Kaze.

Kwa upande wa Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Selemani Matola, alisema fainali ni fainali, mchezo utakuwa wa ushindani mkubwa na anawaheshimu wapinzani wao.

"Ni mechi ya ushindani, hii ni fainali ila zaidi ya fainali kutokana na upinzani wa timu hizi mbili, tunaingia kwa tahadhari na kuhakikisha wachezaji wetu wanafuata maelekezo na kushinda," alisema.

## STARS, DR CONGO ZATOSHANA NGUVU

**Na Adam Fungamwango**

BAO la dakika ya 51, lililofungwa na Ayoub Lyanga, limeikoa timu ya Taifa ya Tanzania kwa kipigo kutoka timu ya Taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na kutoka sare ya bao 1-1 kwenye mechi ya kirafiki ya kimataifa iliyopo kwenye Kalenda ya FIFA, iliyochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana.

Lyanga, alifunga bao hilo kwa kichwa, akiunganisha krosi iliyopigwa na Ditram Nchimbi aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Adam Adam, akimzidi mbio Lusolo Ernest na kumimina krosi iliyotua kwa mfungaji.

Kwenye mechi hiyo ni kama timu hizo ziligawana vipindi, kwani DR Congo, ilitawala zaidi kipindi cha kwanza na Taifa Stars iling'ara cha pili.

Fiston Mayele aliipatia DR Congo bao dakika ya 19 baada ya kupata mpira akiwa nje ya lango, akageuka na kuachia shuti kali lililomchanganya Juma Kaseja ambaye aliteleza na mpira kujaa ndani ya wavu.

Kipindi cha pili Stars ilifanya mabadiliko kadhaa ambayo yaliichangamsha timu na kufanya mashambulizi kadhaa, lakini washambuliaji hawakuwa makini. Kwenye mechi hiyo, beki wa Taifa Stars Aggrey Morris aliagwa rasmi kuichezea timu hiyo huku akikabidhiwa hundi ya Sh. milioni tano kwa mchango wake ndani ya timu hiyo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002